# Nipashe

Ijumaa Novemba 27, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580412

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710




## KIJANA afungwa jela miaka 60 kwa kumpa mwanafunzi ujauzito

UKURASA 3

## JAMII ya Wahadzabe walia eneo kuvamiwa na wafugaji

UKURASA 4



Tumtakie heri Rais Hussein Mwinyi

BUFE

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

MAMBO YA KISASA STENDI MPYA MBEZI

Cleophace Batahe: Hii ndio TUGHE yetu Mwanza katika 'hapa ni kazi tu'

UKURASA 11

# ACT-Wazalendo wapiga kura maoni kuamua SUK

UKURASA 2




Kituo kipya cha mabasi yaendayo mikoani na nje ya nchi cha Mbezi Luis, jijini Dar es Salaam, kimeanza rasmi majaribio. **Picha ndogo:** Baadhi ya mabasi yakiwa yameegeshwa kituoni hapo. **Habari Uk. 4. PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sarakasi za ubunge Viti Maalum wa CHADEMA

**BAVICHA** yataka wafukuzwe uanachama, hatima yao kujulikana leo... *Endelea Ukurasa wa 2*

## EWURA yaanika wenye magari wanavyoibiwa mafuta vituoni

UKURASA 3

**MICHEZO** **MESSI, RONALDO WAMLILIA MARADONA** UK. 21

**MAONI, KATUNI UK. 6**

HABARI KITAIFA

## Ajali yaua sita, akiwamo padri

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WATU sita akiwamo Paroko wa Kanisa Katoliki Parokia ya Masakta Babati, mkoani Manyara, Padri Sixtus Massawe (56), wamefariki dunia baada ya gari walilokuwa wakisafiria kugonga lori kwa nyuma lenye namba RAA 168E.

Gari walilokuwa wakisafiria lenye namba za usajili T.107 BMV Toyota Land Cruser hard Top, ni mali ya Kanisa Katoliki Jimbo la Mbulu.

Aidha, lori hilo lilikuwa na tela lenye namba RL0167 aina ya Mercedez Benz, ambalo liliua limesimama baada ya kupata hitilafu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Salum Hamduni, alisema ajali hiyo ilitokea juzi majira ya saa 8:20 usiku katika barabara ya Arusha - Dodoma katika eneo la Kambi ya Jeshi Sofa Kata ya Meserani Wilaya ya Monduli mkoani Arusha.

Alisema baada ya ajali hiyo watu sita walifariki ambao ni wanaume watano, akiwamo padre huyo na mwanamke mmoja, ambao hata hivyo hawajatambuliwa.

Aidha, aliwataja majeruhi sita ambao ni Francis Gitayane (57), ambaye ni dereva wa gari hilo, Marko Slaa (56), Silas Giani, Patrice Faustine (34), Timoth Faustine na mwenzao aliyejulikana kwa jina moja la Dismas. Wote ni wakazi wa Masakta. Kamanda Hamduni alisema watu wawili waliokuwa kwenye gari hilo walitoka salama.

Miili ya marehemu wa ajali hiyo imehifadhiwa Hospitali ya Wilaya ya Monduli kwa uchunguzi zaidi na majeruhi wamelazwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa Mount Meru.

Alisema chanzo cha ajali hiyo ni uzembe wa dereva wa Toyota Land Cruser na mwendo kasi pasipo kuchukua tahadhari wakati wa usiku.

Alitoa wito kwa madereva kuchukua tahadhari ili kuepusha ajali zisizo za lazima.



Wateja wakichagua mananasi katika soko la Mabibo, jijini Dar es Salaam jana. Tunda hilo, kwa sasa linauzwa Sh. 500 hadi Sh. 1,000 kulingana na ukubwa wake, kabla ya msimu liliuzwa kwa Sh. 2,000 hadi Sh. 3,000. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kura ya maoni ACT kuamua Serikali ya Umoja Kitaifa

**Na Mwandishi Wetu**

VIONGOZI wa Chama cha ACT-Wazalendo wanaendelea na vikao vya kujadili waingie au la katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) Zanzibar, baada ya mchakato wa kukusanya maoni ya wanachama kutoka majimbo ya Unguja na Pemba kukamilika.

Vikao hivyo ambavyo vimekuwa vikifanyika kwa usiri mkubwa hata hivyo, vinadaiwa kuwagawa wanachama makundi mawili, ambapo wapo wanaunga mkono wazo la kuingia katika serikali na wengine wakipinga kwa hoja kuwa halina tofauti na msimamo uliochukuliwa baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 pamoja na uchaguzi wa marudio wa mwaka 2016.

**ACT YAFUNGUKA**

Hata hivyo, alipoulizwa Mkurugenzi wa Habari na Uenezi wa chama hicho Zanzibar, Salum Bimani, kuhusiana na suala hilo, alisema: "Chama bado kinaendelea na vikao vyake kuhusu msimamo wake wa kuingia katika serikali au laa."

Bimani aliyasema hayo, huku taarifa za zisizo rasmi zikieleza kwamba mchakato wa viongozi wa ACT-Wazalendo wa kukutana na wanachama katika majimbo ya Unguja na Pemba ukiwa umekamilika na kazi kubwa inayofanyika hivi sasa ni kufanya uchambuzi wa maoni ya wanachama na kuangalia faida za kuingia katika serikali hiyo na hasara zake.

Akizungumza baada ya kuwaapisha mawaziri, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alisema ametenga nafasi mbili ikiwamo ya Waziri wa Biashara na Viwanda, na Wizara ya Afya, Maendeleo na Jinsia kwa chama cha upinzani, ambacho kimetimiza masharti ya Katiba ya Zanzibar ya kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa mgombea anayepata zaidi ya asilimia 10 ya kura za urais.

"Tumewaandikia ACT-Wazalendo kuteua jina la Makamu wa Kwanza wa Rais, lakini hadi sasa hawajaleta majibu... lakini tusiwasemee kwa sababu muda bado upo kwa mujibu wa katiba," alisema DK. Mwinyi wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuunda Baraza la Mawaziri hivi karibuni.

Kwa mujibu wa matokeo ya uchaguzi, ACT- Wazalendo ina viti vya majimbo manne kwa nafasi ya uwakilishi, lakini kiti kimoja kiko wazi baada ya Mwakilishi Mteule wa Jimbo la Pandani, Abubakar Khamis Bakari, kufariki dunia kabla ya kula kiapo.

Aidha, matokeo hayo ya uchaguzi yameandika historia mpya ya kisiasa Zanzibar, baada ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa mara ya kwanza kuchukua majimbo yote 32 Unguja tangu kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi mwaka 1992 na kurejesha uhai wa CCM kisiwani Pemba baada ya kushinda majimbo 14.

Iwapo Chama cha ACT kitaridhia kuingia katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa, kitakuwa cha pili kujumuishwa katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa kikitanguliwa na Chama cha Wananchi (CUF) baada ya kufikiwa maridhiano kati ya Rais mstaafu wa awamu ya sita, Amani Abeid Karume na Maalim Seif Sharif Hamad kabla ya kufanyika marekebisho ya 10 ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Muafaka uliozaa maridhiano ulitokana na mpasuko wa kisiasa uliojitokeza mwaka 2001 baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2000 na kusababisha zaidi ya watu 30 kupoteza maisha katika maandamano yaliyoitishwa na CUF kupinga matokeo ya uchaguzi mkuu na matukio yaliokuwa yamejitokeza katika uchaguzi huo.

# Hatima sarakasi ubunge Viti Maalum CHADEMA

**Romana Mallya na Christina Mwakangale**

WAKATI hatima ya wabunge wa Viti Maalum wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) inatarajiwa kujulikana leo, Baraza la Vijana la chama hicho (BAVICHA), limetaka wafukuzwe uanachama.

Wabunge hao 19, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake (BAWACHA), Halima mdee, waliapishwa Jumanne wiki hii na Spika wa Bunge, Job Ndugai, katika viwanja vya Bunge, Dodoma.

Mbali na Mdee, wengine walioapishwa ni Grace Tendega, Esther Matiko, Cecilia Pareso, Ester Bulaya, Jesca Kishoa, Hawa Mwaifunga, Tunza Malapo, Naghejwa Kaboyoka, Sophia Mwakagenda, Kunti Majala na Anatropia Theonest.

Wengine ni Salome Makamba, Conchesta Rwamlaza, Angesta Kaiza, Nusrat Hanje, Asia Mohamed, Felister Njau na Stela Fiyao.

Baada ya kuapishwa, Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alisema watachukua hatua dhidi yao kwa sababu hawajawasilisha majina bungeni wala Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Mwenyekiti wa BAVICHA, John Pambalu, akitoa msimamo wa baraza hilo jana, kuhusu wabunge hao, alisema wanaunga mkono msimamo wa chama kwa wabunge hao kwa kuwa waliapishwa kinyume cha mwongozo wa CHADEMA.

Pambalu alisema wanaunga mkono msimamo wa chama kwa wabunge hao kuitwa na hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yao kwa kitendo hicho walichokifanya.

"Tunaunga mkono msimamo wa chama kwa sababu kamati kuu ya CHADEMA ambayo ina uwakilishi wa vijana kwenye kamati hiyo. Katika vikao vyake hatujawahi kujadili, kupitisha orodha yoyote ya wabunge wa viti maalum.

"Kama mjumbe wa vijana sijawahi kukaa na kuwauliza vijana mawazo yao ni yapi baada ya uchaguzi. Kwa hiyo hatujawahi kujadili, wala kupitisha orodha yoyote ya wabunge wa viti maalum, kwa kuwa chama hakijawahi kufanya hivyo wala Katibu Mkuu hawajawahi kusaini kwa yeyote ili kuwa mbunge wa viti maalum.

"Tumeitaka tume ijitokeze hadharani iseme wazi orodha ya viti maalum inayosema ni ya CHADEMA imetoka kwa nani katika mamlaka ya chama hadi ikaifikia tume kuwa hawa ndiyo wabunge wa viti maalum," alisema.

**KAULI YA MNYIKA**

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Mnyika alisema leo kitawaweka kiti moto wabunge hao waliokubali kuapishwa kwa madai ya kutofuata taratibu za chama.

Alisema chama hicho kimeitisha Kamati Kuu Maalum na kwamba watawaandikia wahusika ili kisitokee kisingizio chochote cha kuitwa.

"Nawatangazia kupitia vyombo vya habari kwa wanachama wetu 19 kufika makao makuu ya chama bila kukosa siku ya Ijumaa (leo) saa 2:00 asubuhi, Makao Makuu ya Chama kutoka popote walipo," alisema Mnyika siku hiyo.

Akitoa maoni yake, alipozungumza na Nipashe jana, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalumu, Devotha Minja, ambaye pia ni mjumbe wa Kamati Tendaji ya BAWACHA, alisema hakuna ushirikishwaji uliokuwapo kuwapata wabunge hao.

"Viongozi wa BAWACHA mikoa yote tutakutana kesho, kwa ajili ya kutoa mapendekezo kuhusu hilo," alisema Minja na kuongeza kuwa: "Hatujakaa kujadili ili kuwapata wabunge viti maalum."

Wakati hayo yakiendelea, BAWACHA imetangaza kesho itakuwa na kikao cha ndani na baadaye kuzungumza na waandishi wa habari.

# EWURA yafichua wenye magari wanavyoibiwa mafuta

Na Joseph Mwendapole

MAMLAKA ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) imefichua jinsi wenye magari wanavyoibiwa na watumishi wa vituo vya mafuta wanapokwenda kujaza mafuta.

Imesema ili kuepuka hali hiyo ni vyema wenye magari wadai risiti kila wanapojaziwa mafuta na pia kushuka kwenye magari yao ili kuhakiki kwa makini mafuta yanavyojazwa.

Meneja Mawasiliano wa Ewura, Titus Kaguo, alisema hayo wakati wa mkutano na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari.

Alisema mtu anapokwenda kujaza mafuta anapaswa kuhakikisha kwenye pampu inasomeka alama 00 ndipo aanze kujaziwa mafuta, vinginevyo anaweza kuibiwa.

"Mfano kama kuna mtu kapita hapo kajaza mafuta ya 20,000 na wewe umepita unataka kujaza pengine 50,000 hakikisha alama zile kwenye pampu zinasomeka '00' kwa sababu usipohakiki utajaziwa kwa kuanzia ile 20,000 aliyojaziwa mwenzako," alisema.

Alisema ili kuepuka usumbufu kama huo ni vyema wenye magari wakaachana na kawaida ya kubaki kwenye magari wakiendelea na mambo mengine kwa kuwa hali hiyo inatoa mwanya wa kuibiwa na watumishi wa aina hiyo.

Alisema ili uanze kujaziwa mafuta hakikisha mkono wa pampu umerudi kwenye sehemu yake ya kawaida na hesabu isome 00.

"Kama mkono wa pampu haujarudi kwenye sehemu yake ya kawaida inamaana akikuwekea mafuta unaweza kukuta hesabu inaanzia ile ambayo mwenzako aliyepita amewekewa," alisema.

Mmoja wa washiriki wa mkutano huo, Deodatus Balile, alisema kuna baadhi ya pampu kwenye vituo vya mafuta ambazo zimechoka na haziwezi kukaa kwenye nafasi yake ya kawaida baada ya kuweka mafuta.

Alisema hali hiyo imesababisha watu wengi wenye magari kuibiwa mafuta na baadhi ya watumishi wa vituo vya mafuta bila kujua wanapokwenda kujaza.

## Miaka 60 jela kumpa mimba mwanafunzi

Na Joctan Ngelly, GEITA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Geita imemhukumu mkazi wa Kijiji cha Chibingo, Kasonoko Emmanueli (20), kutumikia kifungo cha miaka 60 jela kwa makosa ya kubaka na kumpa ujauzito mwanafunzi wa darasa la sita.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Samwel Maweda, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha makosa hayo pasipokuacha shaka.

Hakimu Maweda alisema mahakama inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa ili iwe fundisho kwa wengine.

Alisema upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Clemence Kato, ulipeleka mahakamani mashahidi wanne na vielelezo vitatu ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa alimbaka na kumpa mimba mwanafunzi huyo mwenye umri wa miaka 17.

Vile vile, alisema katika tarehe tofauti kati ya Februari na Juni, mwaka huu, mshtakiwa alimbaka mwanafunzi huyo maeneo ya porini.

Hakimu Maweda alisema wazazi wake walipomwona mwanafunzi anabadilika walimpeleka kituo cha afya na alipofanyiwa uchunguzi alibainika kuwa na ujauzito wa miezi minne.

Alisema wazazi walipombana mwanafunzi huyo alimtaja mshtakiwa kuwa ndiye mhusika.

Alisema polisi walimtafuta mshtakiwa huyo na kumkamata na alipohojiwa alikiri kufanya mapenzi na mwanafunzi huyo.




# Wahukumiwa kutumia mtandao wa kilaghai

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imewahukumu Baraka Mtunga na Rajabu Katunda kulipa faini ya Sh. milioni tatu au kwenda jela miaka 2 na kulipa fidia ya Sh. milioni 267.6 baada ya kukutwa na hatia ya makosa ya kutumia mtandao kilaghai.

Kadhalika, washtakiwa wanadaiwa kuisababishia hasara Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ya Sh. 267,656,794.30.

Mbali na adhabu hiyo, mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Kassian Matembele, iliagiza vifaa vya mawasiliano walivyokamatwa navyo washtakiwa vinataifishwa zikiwamo simu mbili na kompyuta mpakato kuwa mali ya serikali.

Hakimu alisema mahakama yake imefikia uamuzi huo baada ya washtakiwa kuingia makubaliano ya kumaliza kesi kwa njia ya majadiliano kati yao na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP).

Akisoma hati ya mkubaliano Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai baada ya pande mbili kukaa na kukubaliana, washtakiwa walitakiwa kulipa fidia ya Sh. 267,656,794.30, lakini walilipa Sh. 200,000,000.

Aliendelea kudai kuwa makubaliano hayo pia yaliwataka washtakiwa hao kumalizia kiasi kilichobaki ndani ya miezi sita.

Akisoma maelezo ya awali katika kesi hiyo wakili Simon alidai washtakiwa hao kupitia kampuni ya Uhuru One ambayo ilikuwa haijasajiliwa kisheria, walitenda makosa ya kutumia na kusambaza huduma za intaneti kwa njia ya kilaghai bila leseni.

Alidai baada ya taarifa za uchunguzi kulifikia Jeshi la Polisi, liliwakamata watuhumiwa ambao walikiri kusimika vifaa vya mawasiliano na kutumia huduma za intaneti isivyo halali.

Pia alidai baada ya uchunguzi zaidi, iligundulika kuwa washtakiwa hao walitenda makosa hayo kati Desemba 13, 2019 na Septemba 28, 2020.

Baada ya kusomewa maelezo hayo, Hakimu Matembele aliwasomea hukumu na kuwaeleza kuwa kwa makubaliano waliyowekeana na DPP na kukiri kwao, nafasi ya rufani imefungwa.

"Nafasi ya rufani inatolewa tu kwa hukumu iliyotolewa baada ya kutiwa hatiani kwa kusikilizwa ushahidi, lakini kwa vile nyie mmekiri baada ya makubaliano, hakuna nafasi ya dhamana," alisema Hakimu Matembele.

Awali washtakiwa hao walikuwa wakikabiliwa na makosa sita ikiwamo utakatishaji fedha ambapo makosa manne yalifutwa na kusomewa hati moja ya mashtaka yenye makosa mawili ya kutumia mtandao kilaghai na kusababisha hasara kwa TCRA.

# Kituo Mbezi Luis chaanza majaribio

**Na Elizabeth Zaya**

KITUO cha mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani cha Mbezi Luis, jijini Dar es Salaam, kimeanza kazi kwa majaribio.

Majaribio ya kituo hicho yalianza juzi kwa gari kuingia, kutoka na kuegesha.

Akizungumza wakati wa majaribio, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abubakari Kunenge, alisema lengo ni kuona gari hizo zitakavyokuwa zinajipanga kabla ya kuanza kutumia rasmi.

Kunenge alisema kituo hicho kimekamilika kwa zaidi ya asilimia 90 na kiko tayari kwa ajili ya kutumika lengo likiwa kuhakikisha wanatekeleza agizo la Rais John Magufuli la kituo kukamilika Novemba 30, mwaka huu.

"Tumefanya majaribio ya kituo cha mabasi cha Mbezi Luis Novemba 25 kwa sababu tunataka kufahamu baada ya shughuli za ujenzi, tuone namna ambavyo magari yanakaa, yanapita wapi, kuna changamoto zipi ili tufanye marekebisho kabla ya Novemba 30."

"Tunataka kuona sehemu ya kupakia abiria, kushusha na kupaki ili baadaye kama kuna maboresho tuyafanyie kazi na kama kutakuwa na hayo maboresho si ya ujenzi, isipokuwa ni namna ya mpangilio wa magari tu, kituo kimekamilika kwa zaidi ya asilimia 90 na kiko tayari kutumika, kituo ni cha kisasa na kitaendesha shughuli zake kisasa zaidi."

Kunenge alisema kituo hicho kitakuwa na uwezo wa kuchukua magari 108 kwa wakati mmoja.

"Lazima tuhakikishe tunajipanga vizuri zaidi na kuna vitu vingi ambavyo vinafanyika kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwamo traffic management, wenye mabasi, na Jeshi la Polisi," alisema Kunenge.

Alisema kabla ya mwisho wa mwezi huu, watakuwa wametoa ripoti kamili ya kuanza kwa matumizi rasmi ya kituo hicho.

"Tunafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha kwamba tunakamilisha agizo la rais la kukamilisha kabla ya mwisho wa mwezi huu," alisema Kunenge.

"Pia jengo hili lina sehemu za shopping mall, parking za mabasi na majengo na tunaendelea na ujenzi wa overnight parking, tutakuwa tunapaki magari zaidi ya 200."

Oktoba 8, mwaka huu, akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa kituo hicho, Rais Magufuli alitoa agizo la kuhakikisha kituo hicho kinakamilika ifikapo Novemba 30.



Mkurugenzi Mkazi wa TradeMark East Africa Tanzania, John Ulanga (kulia), akizungumza katika semina ya umoja wa wanawake viongozi wa baadaye wa Tanzania, iliyoandaliwa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mshauri wa Kimataifa wa masuala ya Teknolojia, Peter Ulanga (kushoto), Mjasiriamali katika Mawasiliano na Teknolojia, Cynthia Bavo (wa pili kulia) na Mjasiriamali Mshauri wa Masuala ya Kidijitali, Kai Mollel. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wanawake Wahadzabe waiangukia serikali

**Na Jumbe Ismailly, Mkalama**

WANAWAKE wa jamii ya kabila la Wahadzabe waishio kitongoji cha Kipamba, wilaya ya Mkalama, mkaoni Singida, wameiomba serikali na wadau wengine kuwasaidia kuwatoa wafugaji waliovamia eneo la pori lililotengwa kwa ajili ya matumizi bora ya ardhi.

Eneo hilo limetengwa kwa ajili ya kuendeleza eneo la akiba na uoto wa asili kwa jamii ya kabila hilo kwa ajili ya mahitaji mbalimbali pia lakini kwa sasa wafugaji wamevamia na kujenga nyumba.

Wanawake hao, wakiwakilishwa na Rabeca Mliga, Apatineko Mashimba na Sima Gonadi, walitoa ombi hilo hivi karibuni Mjumbe wa Kamati ya Misitu, Mathayo Wilson, alipotembelea kukagua msitu huo.

Msitu huo wa hifadhi wanautegemea kwa upatikanaji wa chakula kama vile nyama, mizizi, matunda na asali ambavyo ndivyo vyakula vya watu wa jamii hiyo.

Walisema wafugaji hao ni kutoka jamii wa Wasukuma na Wabarbaig na kwamba baadhi ya viongozi wa vijiji wanahusika kuuza maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya hifadhi.

"Tunasikitika sana kuhusu maeneo haya waliyokuwa wamekabidhiwa kwa ajili ya kutundika mizinga yetu ya nyuki, lakini wameshangazwa baada ya kukuta ujenzi wa nyumba ukiendelea kwa njia za siri," alisema Mliga.

Wilson, baada ya kubaini tatizo hilo, alisema idadi kubwa ya watu kutoka sehemu mbalimbali huingia kwenye maeneo hayo na kuwalazimu kutenga eneo na kujenga pamoja na kuanza shughuli za kibinadamu.

Kutokana na hali hiyo, aliwataka waliovamia eneo hilo la hifadhi ya uoto wa asili, waondoke na kuwatengea eneo la Namba Sita na Masulage ndiko walikotakiwa kuendelea na maisha.

"Tunashukuru serikali kutenga eneo hili dogo na zile akiba akiba kuwamo lakini sasa tunachokiomba hebu watazame hizi akiba ndogo ndogo zisiingiliwe kwa sababu na sisi Wahadzabe tunazaana sana"alisisitiza mjumbe huyo.

Naye Mwenyekiti wa Jamii ya Wahadzabe, Edward Mashimba, alisema alipokuwa kiongozi wa kabila hilo, aliwatengea pori hilo kama akiba yao kwa ajili ya kujipatia matunda, mizizi, asali na nyama kwa wanyama wanaoishi katika pori lakini anasikitika kuona pori hilo kwisha kwa kufyekwa na wafugaji wa kabila la wasukuma.

"Mimi nilikuwa kiongozi wao eneo hili nikaliacha kama akiba za kuweka mizinga yao na akiba ya kuangalia miti yao ya asili kama vile dawa, matunda na chakula. Sasa ninasikitika viongozi wameanza kufanya biashara kwa kuuza maeneo yaliyotengwa," alisema.

TANGAZO

# tigo pesa — Ni Zaidi ya Pesa

## Ada za wateja. Piga *150*01#

| Kiwango (Tsh) | | Ada kwa mteja (Tsh) | | |
|---|---|---|---|---|
| Kuanzia | Mwisho | Kutuma pesa kwenda Tigo Pesa | Kutuma pesa kwenda Mitandao washirika | Kutoa pesa kwa Wakala/ATM |
| 100 | 999 | 15 | 15 | N/A |
| 1,000 | 1,999 | 30 | 50 | 300 |
| 2,000 | 2,999 | 30 | 50 | 400 |
| 3,000 | 3,999 | 50 | 100 | 600 |
| 4,000 | 4,999 | 60 | 100 | 650 |
| 5,000 | 6,999 | 130 | 200 | 950 |
| 7,000 | 9,999 | 150 | 200 | 1,000 |
| 10,000 | 19,999 | 360 | 550 | 1,450 |
| 20,000 | 29,999 | 380 | 600 | 1,850 |
| 30,000 | 39,999 | 400 | 680 | 1,850 |
| 40,000 | 49,999 | 410 | 750 | 2,350 |
| 50,000 | 99,999 | 720 | 1,250 | 2,700 |
| 100,000 | 199,999 | 1,000 | 1,600 | 3,650 |
| 200,000 | 299,999 | 1,200 | 1,900 | 5,300 |
| 300,000 | 399,999 | 1,500 | 2,300 | 6,500 |
| 400,000 | 499,999 | 1,500 | 2,500 | 7,000 |
| 500,000 | 599,999 | 2,200 | 3,200 | 7,500 |
| 600,000 | 799,999 | 3,300 | 4,300 | 8,000 |
| 800,000 | 899,999 | 3,500 | 4,300 | 8,000 |
| 900,000 | 1,000,000 | 3,500 | 6,000 | 8,000 |
| 1,000,001 | 3,000,000 | 5,000 | 6,000 | 8,000 |
| 3,000,001 | 10,000,000 | 5,000 | 6,000 | 10,000 |

| Tukio | Kuanzia | Mwisho | Ada |
|---|---|---|---|
| Kuweka pesa | 1,000 | 5,000,000 | BURE |
| Kutuma pesa kwa mteja ambaye hana akaunti ya Tigo Pesa au akaunti ya mitandao washirika | 1,000 | 1,000,000 | Ada ya kutuma + Ada ya kutoa |
| Kutoa pesa kwa mteja ambaye hana akaunti ya Tigo Pesa au akaunti ya mitandao washirika | 1,000 | 1,000,000 | BURE |
| Kutuma pesa kwenda nchi za nje | 100 | 5,000,000 | Kulingana na kiwango |
| Malipo kwa Tigo Pesa | 500 | 5,000,000 | Kulingana na kiwango |

| Tukio | Ada |
|---|---|
| Kubadilisha namba ya siri | BURE |
| Kuangalia salio/ Taarifa ndogo | 50 |
| Kurudisha muamala uliokosea (Jihudumie) | 50 |
| **Kupata taarifa ya mwezi** | **Ada** |
| Taarifa ya Mwezi jana/Mwezi huu | BURE |
| Taarifa ya Miezi 3 | 1,000 |
| Taarifa ya Mwaka 1 | 2,000 |

Kwa vigezo na masharti ya huduma tembelea tovuti: https://www.tigo.co.tz/tigo-pesa-standard-terms-and-conditions. **Ada zote zimejumuisha kodi zote zinazohusika**
Kwa Ada za huduma nyingine tembelea tovuti; **https://www.tigo.co.tz/tigo-pesa-tariffs**

**Furahia Malipo kwa Tigo Pesa:**


**KUMBUKA:**
1. Unaweza kuweka au kupokea hadi TSh 5,000,000 kwa siku na unaweza kutoa au kutuma hadi TSh 5,000,000 kwa siku, pia unaweza kuhifadhi hadi TSh 10,000,000 kwa wakati mmoja kwenye akaunti yako ya Tigo Pesa, kama usajili wako umekamilika.
2. Onesha kitambulisho chako kabla ya kuweka au kutoa pesa kwa Wakala.
3. Hakikisha taarifa zako za usajili ni sahihi kwa kupiga *106# kisha 2 au piga huduma kwa wateja kwa maelezo zaidi.
4. Hesabu pesa zako na hakikisha salio lako la Tigo Pesa linaendana na muamala uliofanya kabla ya kuondoka kwa Wakala.
5. Kila mara unapotuma pesa, kumbuka kuhakiki namba ya mpokeaji kuepuka kukosea na usumbufu.
6. Hakikisha unahifadhi namba yako ya siri (PIN) kwa usalama. Usimpe wala kumtajia mtu yeyote namba yako ya siri; iwe wakala wa Tigo Pesa, mfanyakazi wa Tigo au mhudumu wa Tigo Huduma kwa Wateja. Pia kumbuka kubadili namba yako ya siri mara kwa mara.
7. Kutuma muamala wa zaidi ya TSh 5,000,000 ni kwa wafanyabiashara waliosajiliwa pekee.
8. Tigo itakupigia kwa 0713800800 au 0713123103 Tu.
9. Kutoa taarifa yoyote dhidi ya udanganyifu Piga simu namba 100 au tuma ujumbe kwa barua pepe kwenda customercare@tigo.co.tz
10. Unaweza kupokea pesa kutoka zaidi ya Nchi 150 duniani

Unaweza kurudisha **muamala uliokosea**, **token ya luku, ku-unbar akaunti yako ya Tigo Pesa** na **kuriseti PIN**

Piga ***150*01#**
chagua **6 (Jihudumie)**
kisha chagua huduma unayotaka

tigo pesa

App yenye urahisi wa kushangaza!




**Fanya malipo ya Serikali**

SUMATRA · TANESCO LUKU · TRA

Pakua kwenye

Google Play · App Store

tigo pesa

Kuwasaliana na huduma kwa wateja,
Piga **100** bure au tembelea duka lolote la Tigo!
Ada hizi ni kuanzia June 2020

tigo

www.tigo.co.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maelekezo ya IGP moto shuleni yafanyiwe kazi

**JESHI** la Polisi limetoa mapendekezo kadhaa, zikiwa ni jitihada za kuchukua katika kukabiliana na ajali za moto zinazotokea kwa kasi kwenye shule nchini.

Mkuu wa Jeshi hilo, IGP Simon Sirro, amesema mfululizo wa matukio ya shule kuteketea kwa moto wamebaini inasababishwa na mambo mengi ikiwamo migogoro ya uongozi kwenye taasisi hizo.

Alisema katika uchunguzi uliofanywa na jeshi hilo, wamebaini kila tukio lina sababu zake, hivyo hakuna sababu ya jumla, na kwamba matukio mengi yanatokana na migogoro ya uongozi kwenye taasisi kutokana na maslahi binafsi katika baadhi ya shule.

Sababu ya pili ni baadhi ya shule kuwa na miundombinu ya umeme na majengo ambayo haijawekwa vizuri, huku akitaja sababu ya tatu akiitaja hujuma ambapo mwalimu anaona haelewani na utawala, hivyo anamua kumtumia mwanafunzi akachome shule.

Jambo lingine alilitaja kuwa ni kwa walimu kuwachapa viboko wanafunzi, hivyo wanaamua kwenda kufanya hujuma kama kuchoma magodoro.

Kutokana na sababu hizo, IGP alitaja maelekezo kadhaa ya kutekeleza ili kudhibiti kasi za matukio hayo, ambayo matokeo yake ni vifo na uharibifu wa mali za shule na wanafunzi.

Kwamba uwekwe utaratibu kwa kila shule kuachwa mwanafunzi mmoja bwenini kwa ajili ya usalama.

Pia jeshi hilo limeelekeza kwamba kila shule kuwe na ulinzi na kujenga uzio ili kupunguza matukio hayo.

Kimsingi, matukio ya mara kwa mara ya moto kwenye shule zetu yamekuwa yakizua mijadala, huku watu wakielekeza hisia mbalimbali kuhusiana na chanzo chake.

Wapo ambao wamekuwa wakitumia hisia kali ikiwamo kudai kuwa kuna hujuma za kisiasa na hata za kidini, lakini tunafarijika kumsikia IGP akitupilia mbali madai ya aina hiyo.

Tunaona kwamba Jeshi la Polisi limefanya jambo jema kwa kufanya ufuatiliaji kupitia utafiti wake ikiwa ni sehemu ya kutekeleza jukumu lake la msingi la kulinda raia na mali zao.

Kasi ya matukio ya moto shuleni yamekuwa yakiibua malalamiko kuelekezwa kwa Jeshi la Polisi; kwamba linakaa kimya bila kuwabaini wahusika na kuwafikisha kwenye mkono wa sheria.

Upo mlolongo mrefu wa matukio ya moto kwenye shule zetu za umma na binafsi katika maeneo mbalimbali ya Tanzania, lakini kwa kutaja machache. Septemba mwaka huu, wanafunzi 10 walifariki dunia kwa ajali ya moto uliounguza bweni la wavulana katika Shule ya Msingi Byamungu iliyopo wilayani Kyerwa mkoani Kagera.


Julai pia kulishuhudiwa matukio makubwa mawili ya moto yakizigusa shule mbili tofauti ambazo zinamilikiwa na dhehebu la Kiislamu.

Tukio la kwanza lilikuwa ni wanafunzi watatu wa kidato cha pili wa Shule ya Sekondari ya Islamic iliyopo Ilala Dar es Salaam walipoteza maisha baada ya shule hiyo ya bweni kuungua moto.

Pia Shule ya The National Muslim Council of Tanzania inayomilikiwa na Kinondoni High School pamoja na Kinondoni College School iliyopo jijini Dar es Salaam iliungua moto yote na kusababisha hasara kubwa. Wiki iliyopita, shule ya wasichana ya Loreto mkoani Mwanza nayo iliteketea kwa moto na kusababisha hasara kubwa kwa wanafunzi.

Tunazishauri shule zote kuzingatia na kutekeleza maelekezo ya Jeshi la Polisi, tukiamini kwamba yatasaidia kupunguza ukubwa wa tatizo kama si kulimaliza kabisa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge

# Ni ushindi kupindua usugu wa kifua kikuu kwa mapana

Na Yasmine Protace

**UGONJWA** wa kifua kikuu umekuwa ukisababisha watu kupoteza maisha, hasa pale wanapochelewa kupata matibabu kwa wakati katika vituo vya afya.

Hivyo jamii imekuwa ikishauriwa kufika kwenye vituo vya afya kuchunguza afya zao na kama watabainika wana tatizo la kiafya, ni rahisi kwao kupatiwa matibabu, hata wakapona.

Mtu anapojulikana mapema ana tatizo fulani, ambalo linamsumbua, ni rahisi kufanikiwa kupata matibabu na kufikia hatua ya kupona anarejea maisha ya kawaida kabisa.

Hivyo, serikali imekuwa ikihamasisha jamii kujenga utamaduni wa kucheki afya zao. Lengo ni kuwasaidia wenye matatizo matibabu ya haraka na wakati.

Katika kuhakikisha inapambana na afya za wananchi kwa kuziweka sawa, serikali nchini kupitia mamlaka zake zinazosimamia afya imeazimia kutokomeza kifua kikuu kwa kuongeza ugunduzi wa wagonjwa wapya wa kifua kikuu na kuwaweka kwenye matibabu.

Kauli hiyo imetolewa na Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Abel Makubi, alipokuwa akifungua mkutano wa mwaka wa Mpango wa Taifa wa Kifua Kikuu na Ukoma uliofanyika jijini Dodoma.

"Uwezo wa nchi kugundua wagonjwa wapya na kuwaweka kwenye matibabu umeongezeka kutoka wagonjwa 62,908 (asilimia 33 mwaka 2015 na kwa sasa kufikia wagonjwa 82,166 (asilimia 59)," anasema Prof. Makubi.

Ni kutokana na hali hiyo, Prof. Makubi anasema kuna maisha ya wananchi takribani 300,000 wakiwamo watoto 45,000 wameponywa kwa kupatiwa dawa kwa wakati na kufuatiliwa kwa usahihi, kati ya mwaka 2015 na sasa.

Juhudi hizo pia zimeweza kupunguza idadi ya vifo vinavyosababishwa na kifua kikuu kwa asilimia hizo 33, kama Profesa Makubi anavyofafanua: "Mwaka 2015 kulikuwa na vifo 30,000 hivi sasa vimepungua hadi kufikia vifo 20,000."

**"Uwezo wa nchi kugundua wagonjwa wapya na kuwaweka kwenye matibabu umeongezeka kutoka wagonjwa 62,908 (asilimia 33 mwaka 2015 na kwa sasa kufikia wagonjwa 82,166 (asilimia 59),"**

Mganga Mkuu anafafanua kwamba, kuna mafanikio katika hatua hiyo ya ongezeko la kasi ya ugunduzi wa wagonjwa wapya na mikakati mbalimbali iliyowekwa na wizara kupitia Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma.

Hapo kunatajwa kuwapo, maboresho ya huduma za ugunduzi wa ugonjwa wa TB na kutoa kipaumbele kwa makundi yaliyoathirika zaidi kama vile kaya zenye wagonjwa, wanaoishi kwenye kaya maskini, magerezani, wachimbaji wadogo na waathirika dawa za kulevya.

"Aidha tumewekeza katika ubunifu mbalimbali wa matumizi ya teknolojia mpya za 'molekyula' za kubaini TB kwa usahihi na kwa haraka" anasisitiza Prof. Makubi.

Mkurugenzi wa Huduma za Kinga kutoka Wizara ya Afya, Dk. Leonard Subi, ana jicho lake linalovutia kuhusu kifua kikuu kwamba, imefanya vizuri kufikia malengo waliyoyaweka unaomalizika mwaka huu.

"Malengo ambayo tulijiwekea ya kupunguza vifo vitokanavyo na kifua kikuu tumeweza kuyafikia, pamoja na kupunguza madhara yanayotokana na ugonjwa huo," anajigamba Dk. Subi.

Anasema serikali imewza kuongeza vituo vya upimaji wa kifua kikuu sugu kutoka kituo kimoja mwaka 2015 hadi 145, hivyo kuongeza wigo wa huduma za matibabu ya ugonjwa huo.

Mkurugenzi wa Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za MItaa, Dk. Ntuli Kapologwe, anasema ofisi yake kwa kushirikiana wizara inayohusiko na afya, katika kipindi cha miaka ijayo imejiwekea mikakati kadhaa.

Hiyo inajumuisha kuwawezesha watumishi katika vituo vya kutolea huduma za afya, ili wawe na ujuzi na uwezo wa kutambua na kutoa huduma kwa wagonjwa wa kifua kikuu.

## HABARI KITAIFA



Mpishi maarufu nchini, Fred Uisso (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu fainali ya shindano la nyama choma lililozishirikisha baa 60 na kuandaliwa na Tanzania Breweries Ltd mwishoni mwa wiki, kwa lengo la kuboresha huduma ya vyakula na vinywaji. Wengine ni Meneja wa Safari Lager, Pamela Kikuli (wa pili kushoto), msaidizi wake, Hassanal Ibrahim Msiha na Ofisa Masoko wa TBL, Eva Mpogolo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafanyakazi benki matatani madai wizi mil. 33/-

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

WAFANYAKAZI wanne wa Benki ya Finca, tawi la Geita wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita wakishtakiwa kwa wizi wa Sh. milioni 33 na kuwasilisha ripoti za uongo za hesabu.

Ilidaiwa katika ripoti hiyo kuwa salio lililokuwa kwenye benki ni Sh. 76,880,300, wakati halali ni Sh. 47,880,300.

Washtakiwa waliofikishwa mahakamani ni Maria Mwakapala (32), kitengo cha mapokezi katika benki hiyo, Philip Dahaye (35), mhasibu, Francis Kazaura (39), meneja na Furaha Twinzi (21), mlipaji mkuu.

Washtakiwa wote kwa pamoja walipandishwa kizimbani jana mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa mahakama hiyo, Obadia Bwegoge.

Waliposomewa mashtaka yao, walikana na wako nje kwa dhamana ya wadhamini wawili wawili ambao walitoa barua za utambulisho kutoka kwa ofisa mtendaji wa kata na mali isiyohamishika yenye thamani ya Shilingi milioni nne kwa kila mdhamini.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Masambu Danieli, ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuomba tarehe nyingine ya kuwasomea washtakiwa maelezo ya awali.

Hakimu Bwegoge alikubali ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Desemba 10, mwaka huu.

Akisoma hati ya mashtaka jana, Wakili wa Serikali, Masambu Danieli, alidai kuwa tarehe tofauti na muda kati ya Januari na Mei, mwaka huu katika Benki ya Finca Tawi la Geita, wilaya na Mkoa wa Geita, washtakiwa wakiwa waajiriwa wa benki ya Finca, wanadaiwa kuiba Sh. milioni 33 mali ya benki hiyo kinyume na kifungu cha 258 (1) na 271 cha sheria ya kanuni ya adhabu sura ya 16 marejeo ya mwaka 2019.

Daniel alidai mahakamani kuwa kosa la pili washtakiwa wote kwa pamoja wakiwa na nia ya kudanganya waliwasilisha ripoti za uongo za hesabu na ripoti yao ilionyesha salio lililokuwa kwenye benki yao katika hesabu ni Sh. 76,880,300 wakati uhalali ni Sh. 47,880,300.

# Wahitimu Mwalimu Nyerere waomba ukumbi wa kimataifa

**Na Romana Mallya**

WAHITIMU wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, wameuomba uongozi wa chuo hicho, kuangalia uwezekano wa kujenga ukumbi wa kimataifa utakaowezesha viongozi wa mataifa mbalimbali wakiwamo waliosoma chuo hicho kufanya mikutano yao.

Wakizungumza jana katika kongamano la siku moja lililokutanisha uongozi wa chuo hicho na wahitimu wa miaka ya nyuma, walisema chuo hicho kina mandhari nzuri ikiwamo kuzungukwa na bandari na ofisi mbalimbali za serikali.

Mhitimu wa mwaka 2016 aliyesomea Shahada ya Uchumi, Frank Kiwovele, alisema kutokana na umuhimu wa chuo hicho katika kuzalisha viongozi mbalimbali ndani na nje ya nchi ni lazima mandhari ya chuo iboreshwe zaidi ili kuendana na ukubwa wake.

Mhitimu Mtunda Juma, aliyewahi kuwa Naibu Spika wa serikali ya wanafunzi chuoni hapo, alisema mafunzo aliyoyapata yamemwezesha kuwa mjasiriamali na sasa anaagiza bidhaa mkoani na kuziuza Dar es Salaam.

Katibu wa kusanyiko hilo, John Muruga, aliungana na wahitimu na kueleza kuwa uwapo wa ukumbi huo kutawezesha viongozi kitaifa na kimataifa wanapokuja Tanzania, badala ya kwenda maeneo mengine wafanye eneo hilo lenye madhari nzuri iliyozungukwa na Bahari ya Hindi.

Naibu Mkuu wa chuo hicho, Prof. Richard Kangalawe, alisema wana mipango ya muda mfupi, kati na mrefu ya kuhakikisha chuo hicho na matawi yake kupitia ardhi waliyopewa kuwekeza miundombinu ya kisasa.

"Chuo hiki ukilinganisha na vingine kipo kwenye mandhari ya ufukweni hapa Kigamboni, tawi la Zanzibar na Pemba, tunawahakikishia ipo mipango mizuri ya kuhakikisha tunafanya maboresho kulingana upatikanaji wa rasilimali fedha, hivi karibuni tutajenga maktaba kubwa yenye uwezo wa kuchukua kwa mara moja wanafunzi 2,500," alisema.

Kangalawe alisema chuo hicho kimekuwa na mchango mkubwa katika taifa ikiwa ni pamoja na kutoa wataalamu, wabunifu na vile vile ushauri wa kitaalamu ili kuchangia maendeleo katika taifa.

Mwenyekiti wa kusanyiko la wanafunzi hao, Simon Simalenga, aliwataka wanafunzi wanaosoma chuoni hapo wasijichukulie poa, kwa sababu wapo marais ambao wanaongoza nchi mbalimbali za Afrika waliosoma katika chuo hicho.

"Wahitimu naomba msijichukulie poa, chuo hiki kimefundisha viongozi mbalimbali kutoka Afrika ambao leo hii ni marais na wengine wastaafu," alisema.

# Serikali yaiagiza TMDA kujengea uwezo watafiti

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeitaka Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), kuhakikisha inawajengea uwezo watafiti wanaochipukia wakiwamo vijana waliopo vyuoni, ili kuongeza idadi ya watafiti na kuleta faida kwa taifa.

Aidha, imeitaka mamlaka hiyo, kufanya majaribio na utafiti wa uhakika wenye viwango vinavyostahili ili kutoa majibu yanayotarajia kwa dawa na vipimo vitakavyosaidia binadamu.

Maelekezo hayo yalitolewa jana, jijini Dar es Salaam na Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Abel Makubi, wakati wa uzinduzi wa mradi wa kuboresha mifumo ya kudhibiti majaribio ya dawa (ASCEND) katika utafiti mbalimbali unaofanyika nchini.

Alisema kwa sasa watahakikisha TMDA na vyombo vyake wanapunguza muda wa kuidhinisha dawa ili kutoa ruhusa ya kutumiwa.

"Kuna kipindi kuidhinishwa kwa dawa au vipimo ilikuwa inachelewa na kufika hata miezi miwili hadi mitatu, najua kulikuwa na changamoto ya kupata watu wa utafiti, lakini kupitia mradi huu itasaidia kujenga mfumo wa kuongeza spidi ya utafiti," alisema Prof. Makubi.

Aidha, alisema TMDA na taasisi ziangalie suala la gharama la kuandikisha utafiti katika kupata matokeo ya utafiti wa dawa zinazoombwa hususani kwa wanafunzi wanaokuwa kwenye masomo vyuoni ambao wengi hawapati fedha nyingine.

Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Adam Fimbo, alisema mradi huo unahusisha taasisi saba za Tanzania Bara na Visiwani ikiwamo Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) na Chuo Kikuu cha Tiba Muhimbili (MUHAS).

Alisema baada ya kuandika andiko la mradi mamlaka imefanikiwa kupata fedha za kuteleza mradi huo kwa muda wa miaka miwili na nusu lengo likiwa ni kuimarisha mifumo ya udhibiti wa majaribio ya dawa, mifumo ya utafiti, namna ya kusoma na kupitisha maombi mbalimbali ya udhibiti wa majaribio ya dawa kabla ya kufanyika nchini.

Alisema pia mradi huo wa miaka miwili utasaidia kuweka mifumo mizuri ya kufuatilia madhara wanayopata watu watakaotumia dawa za majaribio.

Kadhalika alisema kupitia TMDA na MUHAS watatoa mafunzo kwa wataalamu mbalimbali waliopo ndani ya mamlaka ya udhibiti pamoja na wanaofanya majaribio ili kupata uelewa zaidi mpana katika masuala hayo.



Daraja la juu la treni ya mwendokasi likiwa hatua za mwisho kukamilika katika eneo ya Buguruni Tazara, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Pwani, TADB sasa kuwainua wakulima

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKOA wa Pwani kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), imeweka mpango wa kuwainua wakulima kiuchumi, ambapo wakulima 3,000 wananufaika kwa pembejeo.

Wakulima hao wanaolima mpunga katika bonde la Mto Ruvu Halmashauri ya Chalinze wilayani Bagamoyo Mkoa wa Pwani, watanufaika na pembejeo za kilimo.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa Mkoa huo, Mhandisi Evariost Ndikilo, wakati wa makabidhiano ya mkopo wa matrekta mawili pamoja na pembejeo nyingine za kilimo zenye thamani ya shilingi milioni 480 kwa uongozi wa Chama cha Ushirika wa Wakulima wa Umwagiliaji wa Ruvu (CHAURU) ambavyoo vimetolewa na TADB.

Pia aliahidi kuwa katika kufanikisha azma ya mradi wa bonde la Mto Ruvu, ataendelea kuwapa ushirikiano wa kutosha wakulima wa mazao mbalimbali ukiwamo mpunga na kuwahimiza wadau wengine wa sekta ya kilimo kuunga juhudi za serikali katika kuwasaidia wakulima kutimiza malengo waliyojiwekea.

Mkurugenzi wa Fedha wa TADB, Delick Lugemala, ambaye alimwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, alisema lengo lao ni kuwakomboa wakulima kwa kuwapatia mikopo kwa bei nafuu, na kwamba katika Mkoa wa Pwani wameshatoa zaidi ya shilingi bilioni 20.

Alisema benki hiyo itaendelea kushirikiana na wakulima kwa kuwezesha mitaji, ambayo watakuwa wanaipata kwa riba nafuu, lengo ni kuwapatia fursa mbalimbali za kilimo, ambazo zitawasaidia katika kujipatia kipato na kujikwamua kiuchumi.

Mwenyekiti wa Bodi ya CHAURU, Sadala Chacha, alisema msaada huo utawaondolea vikwazo vya upatikanaji wa zana za kilimo na kuwaondolea usumbufu waliokuwa wanaupata awali.

# Wenye ulemavu wapewa elimu ya bidhaa bandia

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KATIBU Tawala wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, Timoth Ndanya, amewataka wenye ulemavu wa kutosikia kuchangamkia fursa ya mikopo isiyokuwa na riba inayotolewa na Halmashauri ya Mji wa Kahama kwa ajili ya kukuza mitaji yao.

Halmashauri hiyo, hutenga asilimia 10 ya mapato yake ya ndani, asilimia nne kwa vijana, nne kwa kinamama na mbili kwa watu wenye ulemavu na mikopo hiyo hutolewa bila riba.

Ndanya alisema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya siku moja ya Tume ya Ushindani (FCC) kwa watu wenye ulemavu wa kutosikia kuhusu majukumu ya Tume na udhibiti wa bidhaa bandia kwa kushirikiana na Chama cha Wenye Ulemavu wa kutosikia (TAMAVITA), mjini hapa.

Alisema, halmashauri zinatenga asilimia kumi ya mapato yao ya ndani kwa ajili ya makundi maalumu wakiwamo walemavu wasiosikia na kuwapatia mikopo isiyokuwa na riba lengo likiwa ni kukukuza mitaji na kuwainua kiuchumi hivyo ni vema wakaendelea kuchangamkia fursa hiyo.

Hata hivyo, Ndanya aliwataka wajasiriamali wenye ulemavu kuendelea kuzingatia maadali ya ufanyaji biashara kwa kuzingatia ubora wa viwango vya bidhaa wanazozalisha ili kuendelea kuongeza wigo wa soko la ndani kabla ya kuanza kufanya biashara nchi za jirani.

Pia, aliwataka kutumia kituo cha uwezeshaji wananchi kiuchumi kilichofunguliwa mjini hapa kwa kuongeza thamani ya bidhaa na kutambua soko la bidhaa wanazotengeneza kwa kuwa serikali inatambua mchango wao katika kuendelea kuijenga nchi kwa kufanya biashara ndogo ndogo.

Mkurugenzi wa kudhibiti bidhaa bandia kutoka FCC, Godfrey Gabriel, alisema kuwa mafunzo yanayotolewa yamekwisha kutolewa kwa viongozi na wanachama wasiosikia katika mikoa ya Tanga, Manyara na Mbeya lengo likiwa ni kudhibiti bidhaa bandia.

Gabriel alisema, wamejipanga zaidi kupeleka elimu ya utambuzi wa bidhaa bandia kwa makundi maalumu ya wenye ulemavu wa kusikia na kuona kwa kuwa ndio makundi yenye changamoto na uhitaji mkubwa zaidi wa elimu ya mlaji na jinsi ya kuepukana na bidhaa bandia. Mwakilishi wa Chama cha Viziwi Mkoa wa Shinyanga, Zawadi Masoud, alisema, Halmashauri ya Mji wa Kahama imefanikiwa kutoa mikopo isiyokuwa na riba asilimia mbili kwa wenye ulemavu wa kutosikia, viungo na watu wenye ualbino na wengi wao wanaendelea na shughuli za ujasiriamali mjini hapa.

Alisema kuwa elimu iliyotolewa ya utambuzi wa bidhaa bandia itasaidia kupunguza changamoto waliyokuwa wakiipata wakati wakinunua na kuuza bidhaa bila kutambua kama ni bandia na kukosa uaminifu kwa wateja wao na kwamba elimu hiyo watawapatia wengine ambao hawakupata nafasi kushiriki.

# Tale aahidi kuchimba visima 14 vya maji



**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

OFISI ya Mbunge wa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki kwa kushirikiana na Bonde la Wami Ruvu, inatarajia kuchimba visima vya maji 14 katika kata za Ngerengere, Mkulazi na Gwata, Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro.

Akizungumza wakati wa ziara ya kukagua maeneo yatakayochimbwa visima hivyo, Mbunge wa jimbo hilo, Hamis Teletale (pichani), alisema kata hizo zilizo pembezoni mwa mkoa zinakabiliwa na changamoto kwa muda mrefu na maji yanayopatikana ni ya chumvi. Alisema hatua hiyo ni kumuunga mkono Rais Dk. John Magufuli ya kutaka kuwatua ndoo kinamama ambao wanatumia muda mwingi kutafuta majisafi na kusababisha baadhi yao kuingia katika migogoro kwenye ndoa zao.

"Dhamira kubwa ni kuwaondolea kero ya maji wananchi hasa huku pembezoni mwa mkoa ambako wanapata maji kwa shida na hata wanayoyapata ni maji chumvi, kwa hiyo tumewaleta hawa wataalamu ili watupe ushauri wa maeneo sahihi ya kuchimba visima," alisema Taletale.

Alitaja kata na idadi ya visima vitakavyochimbwa kwenye mabano kuwa ni Ngerengere (8), Mkulazi (2) na Gwata (5).

Abdusalum Nana, mtaalamu wa maji chini ya ardhi, Bonde la Wami Ruvu, alisema ofisi ya bonde imeshajiandaa kuchimba visima virefu vitakavyowezesha kupatikana maji baridi yasiyo na chumvi.

Alisema wanatambua changamoto hiyo ya maji kuwa ni kero ya muda mrefu katika kata hizo na kuwatoa hofu wananchi kuwa baada ya kubainisha maeneo ya kuchimba visima, zoezi hilo linaenda haraka ili huduma iweze kupatikana.

Naye Diwani wa Kata ya Ngerengere, Kibena Kingu, alisema ujio wa wataalamu hao pamoja na mbunge umeleta faraja kwa wananchi kuwa kero hiyo itakuwa historia kwao kwa kuwatua wanawake ndoo.

"Tunafarijika kuona viongozi wetu wamefika kujionea hali halisi maana wananchi huku wanateseka sana na maji chumvi, kwa hiyo tunamshukuru sana Rais Dk. John Magufuli kwa kutuletea viongozi ambao wanajali wananchi na kutatua kero zetu," alisema.

# Sababu bei ya saruji Tanga Cement kupaa

**Na Beatrice Moses**

KUTOKANA na gharama za uendeshaji kuwa kubwa, Kampuni ya Tanga Cement PLC inakusudia kuongeza bei ya saruji ifikapo Januari 2021.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Reinhardt Swart, ambaye alisema ongezeko la bei ya bidhaa zao ni kutokana na gharama za uzalishaji, ikiwamo manunuzi ya makaa ya mawe, gharama za ukarabati wa mitambo ya uzalishaji saruji.

"Mpango wa kuongeza bei ya ifikapo Januari mwakani kabla ya ongezeko lolote la bei, ni lazima wanahisa wetu wajue na kuridhia. Bei za bidhaa zetu zitaongezeka bei kutokana na ongezeko la gharama za uzalishaji," alisema.

Hata hivyo, Swart alisema licha ya uwapo wa sakata la ongezeko la bei ya saruji nchini, lakini kampuni yake haijaongeza bei toka Juni mwaka huu, na kuwanyooshea vidole wasambazaji wa saruji kuwa ndio chanzo cha bei kupanda. "Nadhani ni vyema tukiangazia wanunuzi wa saruji kwa bei ya rejareja...Hapa tuna aina mbili za uuzaji wa saruji; uuzaji wa saruji wa rejareja unaofanyika moja kwa moja, na pia kumuuzia mteja saruji kulingana na hitaji lake, huku njia nyingine ikiwa mteja kujaziwa saruji kwenye malori," Swart alisema.

AlisemaTanzania ina saruji ya kutosha kuwezesha sekta ya ujenzi kuchanua na haitawezekana ghafla tu kukawa na upungufu wa bidhaa hiyo.

Akizungumzia kuhusu uuzaji wa saruji nje ya nchi, Swart, alikiri wasambazaji wa bidhaa hiyo, Rwanda na Mashariki mwa DRC.

"Ni kweli kwamba baadhi ya wasambazaji wanauza saruji Rwanda na DRC, lakini hii haina maana kwamba saruji yetu inauzwa nje ya nchi zaidi kuliko soko la ndani ya nchi. Madhalani, tunauza saruji yetu kupitia mawakala asilimia tatu nchini Rwanda na DRC. Pia ukiangalia washindani wetu sidhani kama wanauza saruji Kenya ama Uganda, hivyo, tumewaachia mawakala kuuza bidhaa hiyo huko," alisema.

Alisema kampuni hiyo haikuathirika sana na Covid -19, na kwamba inazalisha uzalishaji wa kiasi cha tani 1,200,000 kwa mwaka.

"Ukiangalia kwenye uzalishaji wa saruji wakati wa gonjwa la Cvid - 19 kwa mfano tulipohitaji wahandisi wa kufanya matengenezo ya mitambo yetu toka ughaibuni ilikuwa ni ngumu sana kutokana na mipaka kufungwa," alisema.

Aidha, Swart alivitaja vikwazo ambavyo kampuni yake inakabiliana navyo ni ukosefu wa umeme wa uhakika, ukosefu wa usafiri wa uhakika wa treni ya mizigo toka Shirika la Reli Tanzania (TRC), uwekezaji wa kiwanda kaskazini mwa Tanzania.

"Tanga Cement PLC imekuwa na vikwazo vile vile ambavyo tumekuwa tukikabiliana navyo miaka ya nyuma, miongoni mwake ni upatikanaji wa umeme ambao si wa uhakika, umeme unaotumika hapa kiwandani ni mkubwa sana na mahitaji ya kiwanda ni kupata umeme wa uhakika kwani mitambo inayotumika hapa, ukicheza hata sekunde moja tu inakuwa ni tatizo," alisema.



Baadhi ya wageni waalikwa wakifuatilia uzinduzi wa Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia uliofanyika jijini Dar es Salaam juzi, kwa uratibu wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF). **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kabudi: Mchango wa wanawake bado mdogo

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, amesema licha ya jitihada zinazofanywa katika ushiriki wa wanawake katika sekta ya ulinzi na usalama, mchango wao bado ni mdogo.

Kabudi aliyasema hayo jijini Dar es Salaam, wakati wa mkutano wa kuzindua kikosi kazi cha kuandaa mpango kazi wa ushiriki wa wanawake katika vikosi vya ulinzi wa amani.

Mpango mkakati huo unaandaliwa na Taasisi ya Mwalimu Nyerere na Shirika la Umoja wa Maitafa la Wanawake (UN Women).

Alisema wanahitaji wanawake wengi zaidi katika ulinzi wa amani kwa sababu wanaoathirika zaidi ni wanawake na watoto.

"Vikosi vya wanawake vina uwezo wa kuwa karibu na hao watu kwa kukusanya data na kuwasaidia walioathirika na vita," alisema Kabudi.

Aidha, Kabudi alisema serikali ipo tayari kushirikiana na wadau katika kuhakikisha mpango mkakati huu unafanikiwa kwa kiasi kikubwa.

Alisema Tanzania imekuwa mstari wa mbele katika masuala ya ulinzi na usalama tangu Uhuru, kwa kusaidia nchi jirani na nyinginezo. "Wanawake wana nafasi kubwa katika masuala ya ulinzi na usalama, katika maeneo ambayo wanawake wameshiriki kulinda amani hali imeimarika zaidi," alisema. Mbali na ushiriki katika masuala ya ulinzi na usalama, Prof. Kabudi alisema serikali inazingatia uwakilishi wa wanawake katika masuala mengine, ikiwamo siasa, ambapo idadi ya wabunge wanawake katika Bunge la 12 kwa sasa ni 113, kati yao 24 wameshinda katika majimbo.

Alisema kwa sasa wanawake ni asilimia 4.2 ya walinda amani wa Umoja wa Mataifa. Mwaka jana, jumla ya walinda amani 2,300 walipelekwa sehemu mbalimbali ambapo kati yao 184 walikuwa wanawake. Aidha, alisema Tanzania inajivunia askari wake wa amani kutojihusisha katika tuhuma za unyanyasaji ama kuwaonea raia.

Naye, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Joseph Butiku, alisema kuanzisha kwa mchakato huo kuhakikisha kwamba wanawake wanao mpango mkakati wa kuwawezesha kushiriki katika mambo ya amani, ulinzi na maendeleo.

Alisema mapango huo ni kutekekeza azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa ambao utaidia kuhakikisha wanawake wanashiriki.

Mwakilishi wa UN Women, Hodan Addou, alisema watashirikiana na serikali, asasi za kiraia na Taasisi za wanawake katika kufanikisha mpango mkakati.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, John Jingu, alisema mpango mkakati huo utasaidia ushirikishwaji wa wanawake katika masuala ya ulinzi na usalama.

# Kituo cha kulelea watoto chajikita miradi ya kujikwamua kiuchumi

**Na Elizabeth Zaya**

KITUO cha kulelea watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu cha Mwandaliwa kilichopo Mbweni, Kinondoni jijini Dar es Salaam, kimesema kimejipanga kuanza shughuli za kilimo pamoja na ufugaji ili kujikwamua kiuchumi.

Akizungumza na Nipashe, Katibu wa Kituo hicho, Omari Kyaruzi, alisema wamepanga kuanza kuingia katika shughuli hizo ili kuhakikisha wanajitegemea kwa chakula badala ya kutegemea zaidi kutoka kwa wahisani.

"Tumepata funzo kubwa sana katika kipindi cha corona, asilimia kubwa ya chakula cha watoto katika kituo chetu kilikuwa kinaletwa na wahisani... wengi wao wakitoka nje ya nchi, lakini baada ya kuibuka kwa ugonjwa huu hakikuletwa tena na kutusababishia msukosuko mkubwa," alisema Kyaruzi.

"Tunataka kuanzisha miradi yetu ya kudumu ili hata kunapotokea na majanga kama ilivyokuwa ya corona tusihangaike tena. Kipindi cha nyuma tulikuwa tunafuga kuku na ilikuwa inatusaidia sana katika kuuza na kupata fedha hata kwa mboga tulikuwa hatuhangaiki, lakini baadaye walikufa wote, na ndiyo maana tumeona tuanza tena."

Pia aliwaomba wasamaria wema kuendelea kukisaidia kituo hicho kwa kuwa bado hali ya kiuchumi katika kituo hicho siyo nzuri baada ya kupata msukosuko wa kiuchumi kutokana na wahisani waliokuwa wakiwasaidia kusitisha misaada yao baada ya mipaka yao kufungwa kutokana na janga la corona.

Kyaruzi alisema kusaidia watoto yatima na wale wanaoishi katika mazingira magumu ni miongoni mwa nia njema ya kuonyesha uzalendo na pia ni ibada kwa Mwenyezi Mungu.

"Kituo chetu mtu aliyekianzisha kwa nia njema ya kusaidia watoto hao alifariki, lakini kwa sababu tayari tulikuwa tumeshajitolea kusaidia tulisema hatutakata tamaa, tuliendelea kusali na kumwomba Mungu atusaidie tusiache kutoa huduma hii," alisema.

"Tunashukuru bado tumeendelea kupata nguvu ya kutoa huduma hii na tumesaidia watoto wengi wenye matatizo mbalimbali, na baadhi ya watu wamekuwa wakituunga mkono kufanikisha kazi hii ya kuwasaidia watoto na Watanzania wenzetu."

# Azania Bank yahimiza matumizi 'benki mtandao'

**Na Mwandishi Wetu**

MATUMIZI ya benki mtandao yameelezwa kuwa ni njia muhimu ya kuwawezesha wateja nchini kuweza kunufaika na soko la dunia la bidhaa na huduma.

Mkurugenzi Mkuu wa Azania Bank Limited, Charles Itembe, alibainisha hayo jijini Dar es Salaam jana, wakati akizindua kadi mpya za visa za benki hiyo kwamba matumizi ya kadi hiyo yatawezesha Watanzania kufanya malipo kidijitali kutoka sehemu yoyote duniani.

"Kadi hizi za visa zitawawezesha wateja wetu kutumia mtandao wa visa uliopo popote duniani kufanya malipo na kwa hivyo kunufaika na soko la dunia la huduma na bidhaa," alisema Itembe ambaye alizindua kampeni ya 'Miamala iliyorahisishwa na Azania Bank VisaCard' kama sehemu ya sherehe za kutimiza miaka 25 ya benki hiyo nchini.

Alisema wamezindua aina mbili za kadi hizo za Visa na kuzitaja kama Classic VisaCard na Infinite VisaCard ambazo zitatumiwa na wateja wa kawaida na wale wa daraja maalumu.

"Nia yetu kubwa katika kuleta kadi hizi kwa wateja wetu ni kuboresha huduma za kibenki kwani sasa wanaweza kufanya miamala wakiwa popote penye mtandao wa mashine za Visa ATM duniani pote, lakini pia kufanya malipo kwa mtandao," alisema Itembe.

Naye Meneja wa Benki Mtandao wa Kidijitali wa Azania, Vinesh Davda, alisema kadi hizo za Visa ni suluhisho la kuwapatia wateja huduma za benki popote walipo bila kulazimika kufika katika matawi ya benki hiyo.

"Kadi hizi zinarahisisha upatikanaji wa huduma za kibenki kwa wateja wetu wakiwa mahali popote duniani kwani mtandao wa visa ni mkubwa duniani kote. Tunaamini kwamba wateja wetu watafurahia huduma hii kama huduma muhimu katika kufanikisha shughuli zao za biashara na matumizi binafsi," alisema Davda.



Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), Thomas Ngawaiya, akizungumza na wanahabari jijini Dar es Salaam juzi, akitoa ushauri wa taasisi hiyo kuvitaka vyama vya CHADEMA na ACT-Wazalendo kuruhusu wabunge na wawakilishi kwenda bungeni kuwakilisha wananchi. Kushoto ni mmoja wa viongozi wa taasisi hiyo, Athuman Ally. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Gavana BoT aziagiza taasisi za fedha ulinzi akiba za wateja

**Na Elizabeth Zaya,**
BAGAMOYO

TAASISI za kifedha nchini zimetakiwa kuwa na kitengo cha kudhibiti vihatarishi ili kuhakikisha wananchi au wateja hawapati hasara na kupoteza akiba zao.

Wito huo ulitolewa na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Prof. Florens Lwoga, wakati akifungua kongamano la mwaka la siku tatu la Taasisi ya Kudhibiti Vihatarishi Tanzania (IRMT), lililofanyika jana mjini Bagamoyo mkoani wa Pwani.

Alisema, serikali imeweka utaratibu mzuri wa kuhakikisha taasisi zote za umma zinakuwa na kitengo cha kudhibiti vihatarishi, kwa kuwa vitengo hivyo vinazuia taasisi au kampuni kupata hasara katika kipindi kigumu ambacho wanapitia au majanga ikiwamo majanga kama ya ugonjwa wa corona.

"Tunataka benki zote za Tanzania ziwe na kitengo cha kudhibiti vihatarishi, inasaidia kuangalia namna bora ya kuwasaidia wateja wake, pia wafanyakazi.

Tunaangalia namna nzuri ya kuzisaidia benki kwenye mtaji, utoaji mikopo, ujuzi wa wafanyakazi na mambo mengine muhimu katika uendeshaji benki," alisema Prof. Lwoga na kuongeza:

"Ndiyo maana benki zinaposhindwa kujiendesha kwa kuruhusu vihatarishi kuharibu biashara zao tunazichukua na kuzisimamia, hatutaki watu wapate hasara katika fedha na mali walizohifadhi kwenye benki hizi. Tunasisitiza uwapo wa ukwasi wa kutosha kwa kila benki za ndani na za nje."

Profesa Honest Ngowi, mtaalamu wa uchumi, alisema mada ya mwaka huu wanaangalia umuhimu wa udhibiti vihatarishi katika kipindi hiki baada ya mlipuko wa ugonjwa wa corona.

"Virusi vya corona vilileta athari katika bajeti yetu ya mwaka huu wa fedha, Tanzania haikuathiriwa kwa kiasi kikubwa na virusi hivi, lakini mataifa ya Ulaya na Marekani yameathiriwa sana," alisema Prof. Ngowi.

Rais wa IRMT, Pius Maneno, alisema kuna umuhimu wa kila mtu katika jamii kuwa na tahadhari katika kila kitu anachokifanya kwenye maisha yake hasa biashara. Kwa sababu vitu muhimu vinavyohitajika kuwa na usimamizi wa vihatarishi ni taasisi za kifedha na zile zinazohusiana uwekaji mali kama sekta ya bima.

# Wakulima waitiwa mikopo ya pembejeo

**Na Mwandishi Wetu,**
MPANDA

WAKULIMA wa Mkoa wa Katavi wametakiwa kutumia fursa zinazotolewa na taasisi za kifedha katika kuchukua mikopo ya pembejeo, ili kuwawezesha kufanya kilimo biashara na kukuza pato lao.

Rai hiyo imetolewa na Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Mpanda mkoani Katavi, Alex Massawe, wakati akifungua mkutano maalum na wakulima na wafanyabiashara wa mkoa huo. Massawe alisema benki hiyo imekuwa ikikutana na wakulima wa maeneo tofauti kwa lengo la kutoa elimu ya kilimo biashara ambayo itamsaidia mkulima kuleta tija katika kilimo.

"Hii ni mara ya kwanza kwa NMB kufanya mkutano maalum na wakulima kwa hiyo ni vyema mkaitumia fursa hii ili kupata mafanikio ya haraka," alisema Massawe.

Akizungumzia mikopo ya pembejeo Meneja Mwandamizi wa Kitengo cha Kilimo Biashara, Wogofya Mfalamagoha, alisema benki inatoa mikopo ya pembejeo za aina tofauti kwa wakulima ambapo rejesho lake ni mara moja tu kwa mwaka katika kipindi cha miaka mitatu. "Mathalani tunakupa trekta unafanyia kazi rejesho lake ni moja tu kwa mwaka, sio mnakwenda benki nyingine mnakutana na rejesho la kila mwezi! Sisi tunaangalia nguvu ya uwekezaji iliyofanyika," alisema. Naye Mwakilishi wa NMB Foundation, Rogers Shipela, alithibitisha kuwa taasisi hiyo itaendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa wakulima.




Ukurasa 13

Tumtakie heri Rais Hussein Mwinyi



Ukurasa 12

**MAMBO YA KISASA STENDI MPYA MBEZI**

BUFE

IJUMAA NOVEMBA 27, 2020
Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

# Cleophace Batahe: Hii ndio TUGHE yetu Mwanza katika 'hapa ni kazi tu'

**Na Anthony Gervas, MWANZA**

SUALA au dhana ya kuwapo vyama vya wafayakazi nchini na nje ya mipaka si geni sana. Ila yako yanayofanana kwa kina na mengine tofauti kulingana na majukumu ya chama kimoja hadi kingine.

Kudadavua hayo, Nipashe lilifunga safari hadi katika ofisi za Chama cha Wafanyakazi wa Serikali Kuu na Afya mkoani Mwanza (TUGHE) kudadisi hayo.

Katibu wa chama hicho mkoani Mwanza, Cleophace Batahe, anaeleza undani wake akiitambulisha kwa kauli: "Maana yake ni muungano wa sehemu ya kazi au sekta husika ya kazi. Muungano huu unatokana na ridhaa yao wenyewe kwa madhumuni ya kutafuta, kulinda, kutetea haki na maslahi.

"TUGHE ni ufupisho wa maneno yanayosomeka kwa Kiingereza, 'Tanzania Union of Government and Health Employees' ambayo yalitafsiriwa kwa Kiswahili ili kukidhi matakwa ya wanachama, yaaani Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania."

Batahe anakumbusha kanuni ya chama cha wafanyakazi, ni sharti kukidhi ya ajira na uhusiano kazini ya mwaka 2004, inayosimamia vyama vya wafanyakazi nchini.

### WAKOJE MWANZA?

Katibu huyo wa TUGHE anasema, hadi sasa kuna wanachama zaidi ya 4,200 waliojiunga, pamoja na matawi 75 ya wilaya na mkoa, anahamasisha wafanyakazi kuendelea kujiunga katika chama bila kuogopa zengwe la aina lolote.

"Wanachama wa TUGHE wanatokana pia na wafanyakazi wa sekta za serikali, wakala wa serikali, mamlaka za serikali, mamlaka za maji, sekta ya afya katika serikali za mitaa, taasisi za umma, dini na binafsi zinazotoa huduma za kinga na tiba, magonjwa na bohari ya dawa," anasema Batahe.

Vilevile anasema kuna jumla ya wafanyakazi waajiriwa ndani ya chama hicho, wanaotumikia maduka yanayotoa huduma za dawa na ruksa kwa wote kujiunga ndani ya Mwanza.



Katibu wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali Kuu na Afya (TUGHE), Cleophace Batahe, alipozungumza na Nipashe ofisini kwake, jijini Mwanza. **PICHA: ANTHONY GERVAS.**

### ILIKOTOLEA

Batahe ana simulizi kuwa chama chao TUGHE, kiliundwa baada ya kutokea mabadiliko katika historia ya vyama vya wafanyakazi nchini, yaani kutoka katika mfumo wa chama kimoja cha wafanyakazi NUTA na baadaye JUWATA, uliokuwapo tangu mwaka 1964 hadi 1999.

Mfumo huo wa mabadiliko uliruhusu, wafanyakazi wenyewe kuunda vyama vyao kulingana na sehemu au sekta wanazofanyia kazi, lengo ni kuondokana na mfumo wa chama kimoja.

Anaeleza kwamba, TUGHE ni miongoni mwa vyama huru 11 nchini vilivyoundwa chini ya sheria ya OTTU ya mwaka 1991 na na kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Wafanyakazi ya Mwaka 1998.

Katibu huyo anataja dira lengo walilokuwa nalo ni kuwa chama bora cha wafanyakazi nchini chenye nguvu, kinacholinda, kutetea, kudumisha haki, wajibu na uhusiano kati ya wafanyakazi, waajiri, serikali na sekta ya afya.

Batahe anasema, katika hilo wana mtazamo a kuwaunganisha, kuwaelimisha, kutetea haki, wajibu na maslahi ya wanachama kwa kutumia watumishi makini ndani ya wakati mwafaka.

Pia, ana ufafanuzi kuwa TUGHE inafanya kazi kwa kushirikiana na vyama vingine nchini na kimataifa katika azma ya kuyimiza malengo husika.

### INAFANYAJE KAZI?

Katibu Batahe ana ufafanuzi kuwa, wanaanza kwa kushirikiana na kujadiliana na waajiri, namna ya kudumisha amani kazini, kuboresha na kuendeleza hali bora ya wanachama kazini na baada ya kustaafu.

Pia, anasema wao kama chama wanachukua jukumu la kuondoa tofauti zinazojitokeza kati ya mwajiri na mwanachama au mwanachama mmoja na mwingine, kwa njia ya makubaliano ya amani.

TUGHE Mwanza, kama ilivyo kwingineko wanasimamia utekelezaji mikataba ya hali bora za kazi, tuzo, kanuni mbalimbali kama za nidhamu zinazotumika nchini, wakishirikiana na kubadilishana ujuzi na vyama vingine vya wafanyakazi nchini na nje ya nchi.

Mahali hapo, pia anapotaja ni ulingo wa kutoa elimu kwa wanachama katika mustakabali tofauti kama kubadilishana taarifa kuhusu mishahara, hali za wafanyakazi na taratibu zake za kimataifa na kuwasilisha mrejesho au hoja serikalini katika namna kutunga sheria sahihi za kazi na sera za jamii.

"Madhumuni mengine ni kulinda maslahi ya wanachama kwa kushinikiza serikali kuepukana na uandaaji wa sera ambazo ni hatari kwa wafanyakazi," anasema Batahe na anaongeza:

"Tunatetea na kulinda matakwa ya wanachama, kusuluhisha na kutatua malalamiko au migogoro ya kikazi kati ya mwajiri na mwanachama au baina ya wanachama wenyewe kujadiliana."

Sasa Batahe, anaorodhesha ushindi wa haki zote na maslahi yatokanayo na ajira kutetewa kisheria, huku kukizaliwa mikataba ya hali bora za kazini.

Lingine linatajwa kuwa ni kupatikana elimu na maarifa kutoka kwenye chama, yanayotolewa na kuwa na faida kwa ajira na maisha yake kazini na nje ya kazi.

**ENDELEA UK.12**

BIASHARA

# MAMBO YA KISASA STENDI MPYA MBEZI

- Tiketi kwa mtandao, hakuna wapiga debe
- Neema mpya kuwapaisha wafanyabiashara
- Mkurugenzi Jiji aelekeza jicho lake '100%'

**Na Sabato Kasika**

MRADI wa kituo kikuu kipya cha mabasi ya mikoani na nchi za jirani kilichopo Mbezi Luis jijini Dar es Salaam, kinatajwa kuwa ni moja ya miradi mikubwa inayotarajiwa kuliingizia kiasi kikubwa cha fedha kila mwaka.

Mkurugenzi wake Jiji la Dar es Salaam, Sipora Liana, anasema mradi wa kituo hicho utakapoanza rasmi Jumatatu ijayo Novemba 30, ikiwa imekamilika kwa hatua ya kwanza utaliingizia Sh. bilioni 10 kwa mwaka.

Kwa mujibu wa Liana, fedha hizo zitatokana na makusanyo ya kodi za biashara mbalimbali zitakazokuwa zikifanyika ndani ya kituo hicho kitakachokuwa miongoni mwa vituo bora Afrika Mashariki na Kati.

Mbali na jiji kuvuna kiasi hicho cha fedha, mkurugenzi huyo anasema, kituo pia kinatarajia kutoa ajira zaidi ya 10,000 na kuchochea uchumi kwa Watanzania na taifa kwa ujumla.

Mkurugenzi huyo anasema, huo ni wa mradi wa kimkakati utakaosaidia kuongeza mapato ya jiji hilo, pamoja na utoaji huduma bora ya usafirishaji wa abiria wa ndani na nje ya nchi.

Katika ziara ya ukaguzi wa mradi huo, Liana anasema ujenzi wa kituo hicho ulioanza juzi kwa mabasi machache kabla ya kuanza rasmi Novemba 30.

**FURSA ZA BIASHARA**

Liana anasema, tayari jiji lilishawatangazia wafanyabiashara mbalimbali ambao wanataka kutumia fursa ya kufanya biashara katika kituo hicho wajitokeze kufanya maombi.

Anataja baadhi ya fursa hizo za biashara kuwa ni maeneo ya kutolea huduma za kifedha kwa maana ya benki, maduka ya jumla na ya kisasa, migahawa, maeneo ya wafanyabiashara wadogo na kati na ya kuweka mashine za kutoa fedha za benki-ATM.

"Vilevile kutakuwapo maeneo ya maduka ya bidhaa kama vile vipuri, vifaa vya kielektroniki, vya michezo, maduka ya vitambaa, magodoro, vito, vipodozi, mapambo, saluni na vingine vingi," anasema.

Mkurugenzi huyo anataja huduma nyingine ni za kijamii kama vile kituo cha pili cha usafiri na zahanati ambazo wasafiri watakuwa wanazihitaji.

"Jambo la muhimu ni kwamba, waepuke matapeli ambao wanatumia mwanya huo kuwatapeli wafanyabiashara hao, badala yake watumie njia sahihi kwa ajili ya kupata sehemu ya kufanyia biashara ndani ya kituo," anasema Liana.

Mkurugenzi huyo anasema, waombaji walielekezwa kufuata utaratibu uliowekwa wa kuomba kupitia mtandao anuani walioelekezwa.

Anafafanua kuwa utumaji wa maombi ulianza tangu Novemba 9 na kwamba ulitarajiwa kufungwa juzi na kufuatiwa na uchambuzi wa maombi hayo.

"Wakati huu ambao kituo kinaanza kazi, watu wanaojihusisha na utapeli, wanaweza kuwarubuni wafanyabiashara kwamba, wana uwezo wa kuwasaidia kupata nafasi katika kituo hicho hivyo ni muhimu wawe makini," anasema.

Anasema, uwepo wa kituo hicho ni kuendelea kufungua fursa za maendeleo kwa wakazi wa Wilaya ya Ubungo na jiji kwa ujumla, hivyo hiyo ni nafasi ya muhimu kwa wafanyabiashara na wajasiriamali.

**BILIONI 12 ZAOKOLEWA**

Mkurugenzi huyo anasema, aliwahi kutumia Jiji la Arusha, pia Halmashauri jirani ya Mkuranga, anataja gharama halisi ya mradi huo kuwa ni shilingi za Kitanzania bilioni 50.9 zilizotengwa awali na akafafanua kwamba hakutakuwa na nyongeza ya fedha kwenye mradi huo.

"Hadi sasa tumeweza kuokoa zaidi ya shilingi za Kitanzania bilioni 12 katika hizo bilioni 50.9 zilizotengwa kutokana na usimamizi thabiti wa mradi huo kwa kuzingatia maelekezo ya Rais John Magufuli," anasema.

Pia, anafafanua maelekezo ya rais yalikuwa kusimamia fedha za umma, kwamba Jiji la Dar es Salaam limesimamia na kufanikiwa kuokoa kiasi hicho cha fedha na sasa wanatarajia kuvuna Sh. bilioni 10 kwa mwaka zitakazotoka na kodi.

"Kimsingi, serikali imewekeza fedha nyingi katika miradi yake, hivyo ni muhimu kuona miradi hiyo inasimamiwa vizuri na kuitunza ili kuepusha kusababisha hasara ya fedha iliyotokana na kodi za wananchi," anasema.

Alipotembelea katika ziara ya ukaguzi wa mradi, Rais Dk. Magufuli, alitoa kauli akihisi harufu ya 'ulaji' katika madai ya nyongeza ya fedha za mradi na hivi karibuni, asasi yenye wajibu, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ilitoa taarifa ya ilichobaini.

SOKO KITUONI

Mbali na fursa ndani ya kituo, Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo imejenga soko la wafanyabiashara wadogo wakiwamo mama lishe na baba lishe wa Mbezi Mwisho, pembeni mwa kituo hicho.

Mitazamo ya awali, ni kwambna wakati wajasiriamali walio nje ya eno la stendi wanakadiriwa kuwa jumla ya 700 na eneo jirani la Mbezi Mwisho wanakadiriwa kuwa 1,000.

**WAPIGADEBE BAIBAI**

Tofauti na ilivyo kituo cha mabasi ya mikoani cha Ubungo, wapiga debe ndio wakala wakuu wa kuuza tiketi, stendi mpya ya Mbezi Luis, tiketi zitapatikana kwa njia ya kielektroniki.

Mkurugenzi Liana anasema, mfumo wa ukataji tiketi za mabasi unakuwa kwa njia ya mtandao, kwa ajili ya kurahisisha huduma ya ukataji tiketi kwa wasafiri bila usumbufu wa wapigadebe.

Anasema, mfumo huo wa tiketi kwa mtandao utatatua changamaoto za muda mrefu katika sekta ya usafiri, kwa vile utakuwa na taarifa zote muhimu ambazo abiria anatakiwa kuzijua.

Pia, anafafanua mfumo huo utawawezesha abiria kukata tiketi za mabasi popote walipo kwa simu na kwamba ukataji wa tiketi wa kielektroniki hauhitaji mpigadebe kuelekeza abiria basi la kupanda.

Anasema jiji linatambua juhudi mbalimbali ambazo zimekuwa zikifanyika ili kuwaondoa wapigadebe kituo cha Ubungo, lakini hazijaa matunda, hivyo njia mbadala ni mfumo huo hivyo hawatakuwa na nafasi Mbezi Luis.



Mwonekano wa kituo kipya cha mabasi ya mikoani na nchi jirani kilichopo Mbezi Luis, jijini Dar es Salaam.



Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Sipora Liana, akifafanua jambo katika stendi hiyo.




Mabasi yakiingia kwenye kituo hicho juzi, kilipofunguliwa kwa majaribio. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

## CLEOPHACE BATAHE: HII NDIO TUGHE YETU MWANZA KATIKA 'HAPA NI KAZI TU'

**INATOKA UK.11**

Katibu anasisitiza upekee wa mwanachama mwanamke, katika kuendeleza harakati za ukombozi wa jinsia yake kazini na anasisitiza: "TUGHE itaendelea kupambana kutetea na kulinda maslahi ya wafanyakazi katika Mkoa wa Mwanza na kutoa elimu juu ya wajibu wao, haki pamoja na kutatua changamoto zao zinazowakabili."

**MABARAZA MWANZA**

Anasema, TUGHE mkoani na wilaya za Mwanza, imeunda mabaraza ya wafanyakazi yanayotumika kuwasiliana, kushauri, kuweka viongozi na wawakilishi wanaokaa vikao vya pamoja mara mbili kila mwaka, kwa lengo la kuweka sawa mipango, tathmini na utekelezaji majukumu yao.

"Lakini, upungufu wa fedha ndiyo husababisha vikao kuishia kimoja kwa mwaka, jambo linalokwamisha malengo yetu. Mabaraza hayo yameundwa ikiwamo kujua taasisi mbalimbali za wafanyakazi zilizo chini ya wizara, kulinda na kutetea maslahi yao," anasema Batahe.

Anataja lingine ni wafanyakazi kupewa elimu juu ya uelewa mpana wa maslahi yao, kujua wajibu na kudai stahiki zao dhidi ya mwajiriwa na mwajiri kupitia njia ya mazungumzo mezani.

Ni jambo linalowekeza mazingira bora, mahali pa kufanya kazi, usalama pamoja na ushirikiano wa mashirika mbalimbali ya umma na binafsi na serikali haiwapi motisha zao wafanyakazi bora ili kuwatia moyo wa kuchapa kazi zaidi wanapokuwa kwenye majukumu yao.

"Serikali nayo inatakiwa kuwapa motisha wafanyakazi bora ili kuwatia moyo, waendelee kuchapa kazi zaidi, lakini inakuwa ni ngumu," anaeleza Batahe.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Tumtakie heri Rais Hussein Mwinyi



Siku Rais Dk. Hussen Mwinyi, alipoapishwa. **PICHA: MTANDAO**



**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
jkulangwa@yahoo.com

WATANZANIA ndivyo tulivyo. Kuna wakati Rais wa Tanzania, awamu ya nne, Jakaya Kikwete, kuna watu walisema ni mpole sana, hivyo tunahitaji rais mkali.

Kana kwamba aliitikia mwito huo wa Watanzania hao, Rais Kikwete alipomaliza muda wake, akashiriki kuleta Rais mkali, Dk. John Magufuli. Ni mkali ndiyo, hakuna abishaye.

Hata siku anamtambulisha pale Lumumba, Dar es Salaam, iliko Ofisi Ndogo ya Makao Makuu ya CCM, Kikwete alisema ameleta Rais mkali, tingatinga, na alishaanza kumwaga cheche.

Alipomwaga cheche zikiwamo za utumbuaji majipu, wale wale waliotaka mkali wakaanza kulia na kulalamika, kwamba mtu huyu mmh! Lakini, yeye akasema hana sababu ya kuwa mkali, lakini ana sababu ya kupambana na rushwa na ufisadi.

Akasema amejitoa mhanga kupambana na majipu, kwa ajili ya kuhakikisha wanyonge wanatatuliwa kero zao na hatimaye gurudumu la maendeleo linasukumwa mbele, na wananchi wanaishi maisha mazuri.

Novemba 11 mwaka huu, nilikuwa mmojawa waliofuatilia Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizindua Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Nilimsikiliza vyema kupitia luninga, huku nikijaribu kumlinganisha na kumfananisha na Kikwete na Magufuli, angalau kwa kauli na mwonekano wake, akiwasilisha dira yake ya miaka mitano katika kuiongoza Zanzibar.

Sina haja ya kuachia watu wanipe majibu ya nilichokiona kwake, zaidi ya kusema kwamba niliona mtu kati ya Kikwete na Magufuli. Si mpole, si mkali. Huyo ndiye Dk. Hussein aliye akilini mwangu.

Sikupata maishani kukaa naye ana kwa ana au kutazama naye uso kwa uso zadi ya kumsikia, kumsoma na kumwona kwa mbali, hasa akisimamia wizara muhimu ya Ulinzi na Jeshi la KujengaTaifa, akisheheni utulivu, busara na hekima.

Kama ninavyoendelea kumwona hivi sasa na leo, sikupata kusikia kashfa au makando kando akiwa mbunge au waziri, mpaka anakuwa Rais wa nane wa Zanzibar. Huyu ndiye Rais Hussein.

Nilipomsikiliza katika hotuba yake, hata kwa wengine, sikumsikia akilalamika au kulaumu wapinzani wake alionyukana nao kwenye uchaguzi.

Zaidi, Rais Hussein alisikika akihimiza maendeleo ya Zanzibar, lakini kikubwa, mshikamano wa Wazanzibari bila kujali utofauti wa dini, kabila, itikadi, hata rangi. Akisisitiza kuwa Wazanzibari ni wa moja.

Katika kauli yake, akasema katika kuhimiza umoja na mshikamano, hata uteuzi wake katika kuunda serikali yake, ataangalia sifa, taaluma na utendaji kazi wa mtu na si utofauti nilioutaja hapojuu.

Akasisitiza zaidi kuhakikisha kuwa kisiwa cha Pemba kinapewa kipaumbele cha makusudi, katika suala zima la uwekezaji kiuchumi, kwa kuwa eneo mahsusi kwa ajili ya uchumi wa Zanzibar, tofauti nailivyokuwa nyuma.

Katika hali ya kushangaza, Dk. Hussein akasikika akipongeza awamu saba zilizomtangulia kwa kazi kubwa ilizofanya, na kuwa msingi mzuri kwake wa kuanzia kuijenga zaidi Zanzibar kiuchumi. Anatambua kuwa bila wao, Zanzibar isingefika ilipo.

Akasema anaanzia walipoishia viongozi waliomtangulia. Hiyo ni heshima kubwa katika kutambua mchango wawaliomtangulia, akiwamo baba yake mzazi, Alhaji Ali Hassan Mwinyi.

Kwa upole na ukali alio nao Dk. Hassan, ndiyo sababu hakusita kusema waziwazi anavyokerwa na jinsi bandari ya Malindi na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amaan Karume, vinavyoendeshwa na kuathiri uchumi wa visiwa hivyo.

Pamoja na kuchukua hatua za papo kwa hapo, ikiwamo kufanya uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa Bandari ya Malindi, akaendelea kuahidi kukabiliana na rushwa na ufisadi, mambo ambayo yamekuwa yakikwamisha maendeleo ya nchi.

Hakika Dk. Hussein ameanza vizuri, anachohitaji sasa ni ushirikiano wa wananchi wakiwamo wanasiasa wa vyama vyote, hata vilivyoshindwa katika uchaguzi, kwa kuponesha madonda yaliyotokana na mbigiri za safari ya uchaguzi na kusonga mbele.

Bila shaka upole na ukali wa Dk. Hussein, utaivusha Zanzibar hata kufikia maendeleo yanayotakiwa chini ya sera ya Uchumi wa Bluu, ambao unaonekana kuwa uti wa mgongo wa maendeleo ya visiwa hivyo. Alamsiki!

UCHUMI

# Mabosi wanawake walivyopambana kazini kukabili janga la corona lilipotikisa nchi

## • Ofisini palikuwa pagumu, nyumbani mtihani
## • TEHAMA ilichukua nafasi kuziba mapengo

**Na Jenifer Gilla**

WAKATI nchi imetangaza kuushinda ugonjwa wa virusi vya corona, lakini nyuso zinapogeuzwa nyuma, kuna mambo mengi ya kujifunza kutokana na kadhia iliyopitia katika kipindi hicho.

Ikitimu miezi mitano tangu Juni 29 mwaka huu, Rais Dk. John Magufuli, alitangaza kufunguliwa shughuli zote zilizokuwa zimefungwa tangu Machi 18, ili kudhibiti maambukizi ya virusi vya corona nchini.

Hapo ilihusu zaidi katika shule za msingi hadi vyuo, safari za nje ya nchi na michezo, huku akisisitiza haja ya tahadhari sahihi inayopaswa kuchukuliwa.

Kilikuwa kipindi kigumu kwa Watanzania, kila mmoja akipambana kuhakikisha yeye pamoja na mtu wake wa karibu wanajiepusha na ugonjwa huo.

Wanawake ni moja ya kundi lililokuwa na wakati mgumu katika kipindi cha mlipuko wa ugonjwa wa Covid-19, kutokana na nafasi kubwa waliyo nayo katika familia.



Makamu Mwenyekiti wa Shirika la Maasai Women Development Organization (MWEDO), Dk. Eliamani Laltaika(wa pili kulia), Mkurugenzi wa shirika hilo, Ndinini Kimesera(wa pili kushoto), Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa Arusha, Blandina Nkini(kushoto) na Mjumbe wa Bodi ya Mwedo, Esupat Ngurupa, walipokabidhi misaada ya usafi kwa ajili ya kuunga mkono juhudi za kukabiliana na ugonjwa corona. **PICHA: MTANDAO.**

### YALIYOWAKUTA KINAMAMA

Nipashe ilipata faragha ya kunong'ona na kinamama viongozi katika taasisi mbalimbali, ambao walianika namna changamoto za kiuongozi na kifamilia wamekutana nazo katika kipindi hicho.

Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake nchini (TAMWA), Rose Ruben ana simulizi ya namna hofu iliyoukuwa mtihani mkuu wa kwanza waliokumbana nayo na anasimulia namna walivyohofu kupata maambukizi ya ugonjwa, na hata sura ya umauti ilivyomjia.

"Kwa hiyo, changamoto niliyoipitia ni namna ninavyoweza kuwasaidia wafanyakazi wangu pamoja na familia zao ili waepuke ugonjwa huo, lakini familia yangu na mimi mwenyewe niwe salama," anasema Rose.

Pia, anataja mtihani wa pili unaomkabili ni uhaba wa vitendea kazi wawapo majumbani, huku walikabiliwa na shida ya mtandao zilizowapunguzia kasi ya utendaji kazi.

Anaeleza kwamba, hilo lilitokana na kutii agizo la serikali la kutaka watu wafanye kazi majumbani kuepuka misongamano inayoweza kuongeza kasi ya maambukizi ya maradhi ugonjwa.

"Hii iliathiri sana utendaji wetu, kwa maana ya kwamba tulikuwa hatumalizi kazi kwa kipindi tulichokitarajia, kutokana na changamoto kama hizo hasa za kimtandao," anasimulia.

Kuahirisha shughuli za maendeleo zilizohitaji kukutana ilikuwa ni lingine analolitaja Rose, msukosuko wa utendaji wake wa kazi, wakati huo, hata alilazimika kusitisha mikutano yote waliyopanga kufanya na wadau mbalimbali wakiwamo wafadhili.

Ni jambo analolitaja kumrudisha nyuma maendeleo ya ofisi, pamoja na kuitia taasisi hasara, kutokana na gharama walizotumia kuandaa baadhi ya mikutano, ikiwamo kulipia kumbi.

Mkurugenzi wa Tanzania Young Women Leaders, Consolata Chikoti, anakuja na malalamiko ya madhila yake akianza na maelezo yanayofanana na mtangulizi wake, Rose, alipotingwa na hofu kwamba, huenda angepata maambukizi ambayo yangeifikia familia na hasa mwanawe ambaye ni viguu kutengana naye.

"Ukiwa mwanamke 'automatic' (moja kwa moja) unakuwa 'caretaker' (mlinzi na mwangalizi), hasa ukiwa na mtoto mdogo wa kunyonyesha ndio kabisaa! "Hii ilikuwa inanikosesha raha kila ninapokuwa naelekea nyumbani baada ya kutoka kazini, nawaza naweza kumwambukiza mtoto ugonjwa huu.

"Ilinibidi niwe naingia nyumbani kwa kujificha ili mtoto asinione na kunililia, nihakikishe nimeoga na kubadilisha nguo ndipo nimhudumie. Kwa kweli ilikuwa changamoto kubwa kwangu hasa kiutendaji," anasimulia Consolata.

Mama huyo mtaaluma wa sheria, pia anataja mazingira ya kufanya kazi majumbani hayakuwa rafiki na kuna wakati ilimwita mtihani kushika nafasi ya uongozi na mama wa nyumbani kwa wakati mmoja.

Anaendeleza ushuhuda, akisema kuna kipindi ilibidi kuachia jukumu la kiuongozi, ili amhudumie mtoto aliyekuwa akimlilia wakati alipoendelea na jukumu hilo.

"Ni ngumu sana kufanyia kazi nyumbani kama una mtoto mdogo, kila anapokuona analilia kuwa karibu na wewe, umbebe, umnyonyeshe, hata nilipojaribu kujificha kilio chake kikizidi uzalendo ulikuwa unanishinda.

"Kuna wakati nilikuwa nasimamisha mkutano kwa muda, nawaomba radhi wafanyakazi wangu wanipe wasaa kidogo nimhudumie mtoto," anasema.

Mkurugenzi wa Global Peace Foundation (GPF), Martha Nghambi, ana maelezo kwamba, kitendo cha kujifungia ndani na kutofanya shughuli kama zamani kilimkosesha amani

Kwa mujibu wa Martha, kitendo cha kutoruhusiwa kuwatembelea ndugu, jamaa, marafiki kiliwafanya watoto wake wakose furaha, hali iliyomuumiza hata yeye.

"Kikubwa ni kukosa amani na furaha kuona watoto hawaendi shule, japo baadaye waliendelea na masomo kwa njia ya mtandao lakini hata wao walikuwa hawana furaha.

"Pia, kufanya shughuli za kiofisi pamoja na kusimamia watoto wasome na kufanya 'homework' kwa njia ya mtandao, ilikuwa changamoto kubwa kwangu, nilikuwa nachoka sana," anasema.

Sambamba na hilo, kitendo cha kukaa nyumbani pasipo kufanya mazoezi na kutembea, Martha anaeleza ilimkwaza hata kisaikolojia.

### NAMNA WALIVYOKABILI

Katika kupambana na kadhia ya kushinda na usumbufu wa nyumbani, Consolata anaeleza alilazimika kufanya kazi sehemu nyingine. akichukua umakini maradufu, akizingatia tahadhari zote zilizotangazwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Pia, kutoka TAMWA, Rose anataja mbinu aliyotumia kupambana na hali hiyo, ni kuhakikisha anahamasisha wafanyakazi pamoja na familia yake kuchukua tahadhari iliyotolewa na Wizara ya Afya, ikijumuisha kunawa mikono na kutumia vitakasa mikono.

Anataja mengine kwa msisitizo, inajumuisha kuvaa barakoa wanapokuwa kwenye mikusanyiko ya watu, pia kutumia TEHAMA kufanya mikutano wakiwa nyumbani ili kuepuka misongamano.

Mkurugenzi huyo alitumia mbinu hiyo hata katika familia yake, ikiwamo kutoa somo kwa wanafamilia na kuweka vifaa vya kujikinga nyumbani kwake.

"Hiyo ndio hatua ya kwanza nilikuwa ninaichukua, lakini kama kiongozi bado nilikuwa na hofu," anasema na kudadisi kwa maswali: "Je, watu hawa wameelewa somo la kujikinga na Covid- 19?

"Wanafuata haya maelekezo ninayowapa? Je, ni kweli wanavaa barakoa wanapokuwa kwenye daladala, kwenye mikutano wanatumia kweli vitakasa mikono?"

### ULINGO WA DARASA

Mhariri Mkuu wa gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe, anasifu uwapo wa teknolojia ya habari na mawasiliano au maarufu TEHAMA kwamba ulichangia kwa kiasi kikubwa kupunguza maambukizi ya ugonjwa corona. ULIPOSHAMBULIA NCHINI

Kwa mujibu wa Bandawe, kutokana na teknolojia hiyo kasi ya utendaji katika ofisi yake changamoto ya kutokukutana kufanya mikutano haikuathiri utendaji kazi, kwa sababu walitumia TEHAMA kuendesha mikutano.

"Nimejifunza kuwa TEHAMA ina mchango mkubwa katika maendeleo ya taifa. Imechangia kwa kiasi kikubwa kutoyumba kwa shughuli za kiutendaji katika kipindi hicho, kwa kuwa ofisi nyingi zilihitajika kupunguza misongamano" anasema

Ni aina ya mtazamo unaofanana na kauli ya Mkurugenzi wa TAMWA, Rose, anayeungana kubariki umuhimu wa teknolojia hiyo, hasa katikara kipidi hicho, akitamka: "Kwa kweli TEHAMA imetusaidia sana, nafikiria kama teknolojia hii isingekuwapo mambo sijui yangeendaje."

Mkurugenzi wa Taasisi ya GPF, Martha ana mtazamo wake kuhusu somo la zama hizo, akieleza funzo alilolipata katika kipindi hicho, ikiwamo kutumia magumu yaliyowafika kujifunza kitu kipya, kusaidia wengine na kuwapa moyo.

Ana mtazamo wake wa jumla ni kwamba: "Funzo nililolipata ni kutumia changamoto kama fursa, katika kipindi hicho GPF tulitumia vyema changamoto hiyo, kwa kujifunza kutengeneza barakoa ambazo tuligawa bure kwa watu wasiojiweza na walemavu."

Consolata, anadokeza kwamba amejifunza tayari muda wowote tatizo linapotokea, kwanza kulikubali mapema na kuishi nalo, kwa sababu kadri mtu anapolikataa ndipo linamkwamisha kusonga mbele.

### RIPOTI MFUKO HABARI

Kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa na Mfuko wa Kusaidia Wanahabari Wanawake (IWMF), kukosekana wanawake katika habari zinazohusu Covid-19, kunawaathitri kinamama hao kiuchumi na kisaikolojia, kutokana na mzigo mkubwa wanaoubeba wa kuangalia familia.

Hiyo inatajwa inatokana na uhalisia wa kanuni za kijamii zenye mfumo dume, kivuta unyanyasaji wa kijinsia, kukosekana huduma za msingi, ama kukimbiwa au kutengwa pale wenza wanapothibitika kufa kwa ugonjwa huo.

Pia, ripoti hiyo inafafanua kuwa pamoja na changamoto zote anazopitia mwanamke katika kipindi hicho, bado uwasilishwaji wake katika vyombo vya habari ni mdogo, ikiwa na mfano hai kati ya habari zote zinazohusu corona zilizoandikwa nchini Kenya, wanaume walichukuliwa maelezo mara tatu zaidi.








Mchoraji akiandika maandishi kwenye bajaj iliyoegeshwa barabarani katika barabara ya CDA, jijini Dodoma jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama wake. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# Watumishi mawasiliano watakiwa kuelewa vikwazo vya uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WATUMISHI wa sekta ya mawasiliano wametakiwa kuwa na uelewa wa kubaini na kudhibiti vihatarishi vinavyokwamisha utekelezaji wa malengo ya sekta hiyo.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Mawasiliano), Dk. Zainab Chaula, aliyasema hayo alipokuwa akifungua mafunzo ya siku tano kwa wataalamu wa sekta hiyo ya kuandaa rejista ya vihatarishi, jijini hapa. Aliwataka kuhakikisha malengo ya sekta yanatekelezeka kwa kudhibiti vihatarishi vinavyosababisha malengo hayo yasitimie, ikiwamo upelekaji wa mawasiliano ya uhakika nchi nzima. "Sekta hii ndiyo yenye dhamana ya kusimamia na kusambaza Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano hivyo watendaji mnatakiwa kujipanga kuhakikisha miundombinu hiyo ipo salama dhidi ya uharibifu na kuhakikisha serikali haipati hasara," alisema.

Aidha, Dk. Chaula aliwasisitiza watendaji wa sekta hiyo kutokariri takwimu na kuwataka kuziboresha mara kwa mara ili kupata takwimu halisi ambazo zitasaidia kupima utendaji wa sekta.

Naye, mwezeshaji wa mafunzo hayo, Dk. Ernest Mwasalwiba, kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe, aliipongeza Sekta ya Mawasiliano kwa kuandaa rejista hiyo ambayo itasaidia kufikia malengo iliyojiwekea.

"Kuandaa rejista ya vihatarishi ni hatua ya mwanzo kabisa na haitakuwa na maana kama vihatarishi hivyo havitafanyiwa kazi ya kuvidhibiti visitokee ili sekta kutimiza malengo yake," alisema.

Mratibu wa mafunzo hayo ambaye ni Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Sekta hiyo, Joyce Christopher, alisema uandaaji wa rejista hiyo ni muendelezo wa utekelezaji wa mfumo wa kusimamia vihatarishi vya sekta hiyo ili kuendana na matakwa ya serikali katika ya kubaini na kudhibiti vihatarishi ili kufikia malengo.

# Wapewa angalizo kufanya biashara maeneo hatarishi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAFANYABIASHARA wa matunda na mboga katika soko la Sabasaba jijini Dodoma, wametakiwa kutii maagizo ya Halmashauri ya Jiji hilo, kwa kujiepusha kufanya biashara kwenye maeneo yanayohatarisha usalama wao.

Mwenyekiti wa wajasiriamali wanawake wa soko hilo, Anna James, alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akizungumza na wafanyabiashara hao walipotembelewa na Ofisa Masoko wa Jiji hilo, James Yuna.

Alisema wafanyabiashara hao wanaendelea kuongezeka kwenye maegesho ya daladala, jambo ambalo linahatarisha usalama wao kwa kuwa si eneo sahihi la wao kufanyia biashara.

"Eneo la maegesho ya daladala limekuwa finyu kuna wakati daladala zinalazimika kuegeshwa nje kwa sababu tu eneo linalopaswa magari yaegeshwe limevamiwa na wafanyabiashara, yaani hata mtu haogopi tairi ya gari inapita jirani na alipopanga bidhaa zake," alisema. Alisema kinachofanyika ni wafanyabiashara kukaidi maelekezo, sheria na kanuni zilizowekwa na Jiji kwa kufanya biashara kwenye mpangilio mzuri na eneo ambalo ni salama kwao.

"Kinamama ninawaomba tuiunge mkono Halmashauri yetu ya Jiji la Dodoma kwa hili ambalo lipo kwa ajili ya usalama wetu, tuwe tayari muda wote kutoa ushirikiano kwa vitendo na maelekezo yatakayotolewa ikiwamo hili la kupisha eneo hili la stendi ya Sabasaba, ili daladala ziwe zinafanya kazi yake kwa uhuru na uwazi kwenye eneo hili," alisema.

Kwa upande wake, Ofisa Masoko, James Yuna, alitoa rai kwa wafanyabiashara waliopo stendi ya Sabasaba kufanya shughuli zao kwa mpangilio, ili kuepukana mwingiliano kati yao na waendesha daladala.

"Mkipangilia vyema mtafanya biashara zenu kwa uhuru tofauti na ilivyohivi sasa, ambapo mnapanga ovyo bidhaa zenu hadi kwenye maegesho ya magari na kuwanyima uhuru waendesha daladala," alisema.

Kadhalika, aliwataka wachoma mishikaki, mahindi mabichi na wapika chips, ambao wanaofanya biashara hizo katikati ya magari yanayotumia nishati ya mafuta kuangalia usalama wa eneo hilo kwa kuwa wanaliweka hatarini. "Ni rai yangu wafanyabiashara wote kuendelea kutii maelekezo kwa kuwa ni njema inayowataka wanaofanya shughuli zaokuzingatia vigezo vilivyoelekezwa katika kila eneo hivyo tunaomba ushirikiano kutoka kwao," alisema.

# Prof. Gabriel afunda wanachuo Hombolo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Elisante Ole Gabriel, amewafunda wanafunzi wa Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo jijini Dodoma namna ya kuwa viongozi wanaokidhi matarajio ya Watanzania.

Prof. Gabriel alitoa somo hilo alipokuwa akiwasilisha mada iliyohusu nafasi ya viongozi wa kuchaguliwa katika kuleta maendeleo kwa jamii anayoiongoza kwenye hafla ya kuwatunuku zawadi wanafunzi waliofanya vizuri katika masomo yao na wafanyakazi bora wa chuo hicho.

Alisema katika kipindi ambacho nchi ya Tanzania imeingia katika uchumi wa kati viongozi wanawajibu mkubwa wa kuhakikisha wanakidhi matarajio ya Watanzania.

Prof. Gabriel aliongeza kuwa nchi nyingi na taasisi zimekuwa zikikwama kufikia malengo tarajiwa kwa sababu ya kukosa usimamizi mzuri.

"Kuwa na rasilimali ni jambo moja, lakini kusimamia rasilimali hizo ni jambo la muhimu zaidi, taasisi nyingi zimekwama kwa kushindwa kusimamia rasilimali zake ikiwamo rasilimali watu, rasilimali fedha na rasilimali miundombinu," alisema Prof. Gabriel.

Aliupongeza uongozi wa Chuo cha Hombolo kwa kusimamia ajenda ya uongozi huku akisema kuwa elimu hiyo wanayoitoa kwa wanafunzi wa chuo hicho itawasaidia wanafunzi hapo mbeleni watakapokuwa viongozi.

Alisema kiongozi yeyote wa kuchaguliwa au kuteuliwa ili awe kiongozi bora, ni muhimu kuzingatia mambo matatu ambayo ni kufahamu hasa anaoawaongoza wanamahitaji gani? Pia kiongozi atambue kuwa hatakumbukwa kwa cheo chake bali kwa mchango wake kwa jamii ile anayoiongoza na tatu, awe mtu anayewashirikisha wale anaowaongoza katika kutatua kero zao.

"Washirikishe wale unaowaongoza na ndipo utakapoweza kutatua kero, kiongozi mzuri ni yule anayeona tatizo na kuzibadilisha kuwa fursa, na kwa kufanya hivyo ndipo utaweza kukidhi matarajio ya wale unaowaongoza," alisisitiza Prof. Gabriel.





# Vijana waanza kunufaishwa kazi za mikono

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

BAADHI ya vijana kutoka Halmashauri ya Jiji la Mbeya wameanza kunufaika na ubunifu na kazi za mikono za utengenezaji wa bidhaa mbalimbali zinatokana na malighafi, ambazo zinazalishwa nchini.

Wakizungumza na Nipashe maeneo wanakofanyia shughuli zao, walisema ubunifu wao si tu kwamba umeanza kutimiza malengo yao na kuwa chachu katika kuongeza kipato chao, bali umeongeza fursa za ajira kwa vijana wenzao na kuchangia katika uchumi wa nchi.

Joyce Chavala, mkazi wa Isyesye jijini la Mbeya ni miongoni mwa vijana wa kike ambaye amejiajiri kupitia mradi wake wa utengenezaji wa bidhaa mbalimbali zikiwamo sabuni na mikoba. Alisema kuwa alianzisha mradi huo baada ya kupata mafunzo ya stadi za maisha kutoka kwenye taasisi zinazosaidia vijana na amekuwa akithubutu kutafsiri maarifa hayo kwa vitendo.

"Nalishukuru Shirika la Shop kwa kushirikiana na Foundation for Civil Society kunipatia mafunzo ya kujitambua na ujasiriamali ambayo yamenisaidia kujiajiri kwa kuanzisha kiwanda changu kidogo cha kutengeneza sabuni, na sasa nimeajiri na vijana wenzangu... hakika nimeona mafanikio kwangu na familia yangu, sikuwa hivi awali," alisema Chavala.

Upendo Yohana, mkazi wa Ilemi ambaye anatengeneza mazulia, alisema Tanzania ina fursa nyingi ambazo zitachochea mabadiliko chanya kwa vijana wenye uthubutu wa kufanya kazi kwa ajili ya maendeleo yao kuanzia kwenye kaya hadi ngazi taifa. Mratibu wa shirika hilo, Maria Dominick, alisema SHOP ni baadhi ya mashirika yasiyokuwa ya kiserikali yanayosaidia kuunga mkono jitihada za vijana kujikwamua kiuchumi.

Sambamba na kuwasaidia vijana kujikwamua kiuchumi, alisema pia wanahamasisha watu kufanya kazi kama njia ya kusaidia makundi ya vijana kubuni fursa za ajira, ili kupungua utegemezi.

Alisema zaidi ya vijana 300 katika Jiji la Mbeya wamejengewa uwezo wa kazi za mikono kupitia mradi wa kuwawezesha vijana ambao ulitekelezwa na shirika hilo kwa kushirikiana na Shirika la The Foundation Civil Society (FCS)

"Uthubutu wa vijana hawa si tu kwamba unawanufaisha wenyewe, bali unasaidia kupunguza changamoto za maisha hata kwa vijana wenzao ambao sasa wanapata fursa za ajira isiokuwa rasmi kupitia miradi inayobuniwa," alisema Dominick.

# TMDA, nchi jirani kukabiliana na bidhaa bandia

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), imeahidi kuongeza ushirikiano na nchi jirani katika mapambano dhidi ya uingizwaji wa dawa bandia na duni sambamba na kukagua ubora wa dawa.

Mratibu wa Ofisi za Kanda za TMDA, Dk. Henry Irunde, aliyasema hayo jana wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya wakaguzi wa dawa ngazi ya halmashauri ambayo iliwahusisha waganga wakuu, wafamasia na madaktari wa binadamu na mifugo kutoka halmashauri na wilaya zote za Mkoa wa Mbeya.

Dk. Irunde alisema moja ya mambo yanayochangia uingizwaji wa dawa na vifaa tiba bandia ni kutokuwapo kwa ushirikiano thabiti katika kudhibiti uzalishaji na uingizwaji wa bidhaa hizo ambazo huingizwa nchini kwa njia ya panya.

"Kwa kutambua umuhimu wa ushirikiano kati ya Tanzania na jirani zake, TMDA inakuja na mkakati wa kukaa meza moja kujadili ni kwa namna gani wataweza kudhibiti uzalishaji na uingizwaji wa bidhaa zilizopigwa marufuku," alisema Irunde.

Aidha, aliwaomba wakaguzi 57 ambao wanaopatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo wakaguzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi kuzingatia maadili ya kazi katika kukabiliana na vifaa tiba bandia na utoaji wa taarifa kuhusiana na bidhaa hizo.

Kaimu Meneja wa TMDA, Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Anitha Mshighati, alisema moja ya mikakati waliyoiweka ni kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika mipaka ya Tunduma na Kasumulu ili kudhibiti uingizwaji wa dawa bandia. Alisema kwa kuwa wakaguzi hao ni watendaji wa halmashauri, anaamini baada ya mafunzo hao watakwenda kukabiliana na kudhibiti mianya yote ilikuwa inatumika kuingiza bidhaa zilizopigwa marufuku.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Agness Buchwa, alisema uwekezaji wa viwanda vya vifaa tiba nchini utasaidia kupunguza tatizo la dawa na vitendanishi bandia nchini.

Alisema hadi sasa Mkoa wa Mbeya una jumla ya viwanda vitatu vya kutengeneza vitakasa mikono ambavyo kimsingi havikidhi mahitaji, na kwamba hitaji ni ujenzi wa viwanda vya kutengeneza dawa. Aliwaomba wawekezaji kuchangamkia fursa ya uwekezaji katika dawa, ili kukabiliana na tatizo la bidhaa zilizopigwa marufuku ili kuokoa maisha ya wananchi.

Mmoja wa wakaguzi waliopata mafunzo hayo ambaye ni Mganga Mkuu Hospitali ya Wilaya ya Chunya, Dk. Felister Kisandu, alisema ameongeza maarifa ya kubaini upungufu uliyokuwa kwenye dawa hivyo atakwenda kutoa elimu kwa wananchi kuacha matumizi ya dawa, ambazo zilipigwa marufuku au kumaliza muda wake.

James Mwangolombe, mfamasia wilayani Kyela, alisema moja ya matatizo yanayokwambisha utendaji kazi wilayani humo ni uingizwaji bidhaa kwa njia za panya. Alisema mara kadhaa wamekuwa wakikabiliana na hali hiyo na kwamba kwa sasa amejifunza mbinu za namna ya kwenda kudhibiti njia za panya, lakini kuwaelimisha wananchi juu ya athari za matumizi ya bidhaa hizo.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Busokelo, Dk. Christopher Mwasongela, alisema jamii bado haina uelewa juu ya matumizi ya dawa zenye mwelekeo wa kulevya.



Wananchi wa vijiji vya Ukwavila na Uturo, katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, wakiendelea na ujenzi wa banio la skimu ya umwagiliaji jana, ambapo kwa nguvu zao wamechangia kiasi cha Sh. milioni 175, zinazohitajika ni Sh. milioni 220 ili ujenzi huo ukamilike. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Skimu za umwagiliaji Mbarali kuboreshwa

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WABUNGE wawili mkoani Mbeya wamemtembelea Stella Kalinda (32), mkazi wa Kijiji cha Idendeluka katika Kata ya Sangambi, wilayani Chunya ambaye alijifungua watoto wanne kwa mpigo hivi karibuni na kumpatia msaada kwa ajili ya malezi ya watoto hao.

Wabunge hao ni wa Jimbo la Lupa, Masache Kasaka na wa viti maalumu, Maryprisca Mahundi, walimtembelea mama huyo juzi katika Hospitali ya Wilaya ya Chunya, alikolazwa na watoto hao kwa uangalizi.

Wakizungumza baada ya kumpatia msaada mama huyo, wabunge hao waliwaomba Watanzania kuendelea kumsaidia mwanamke huyo kutokana na gharama ya malezi ya watoto kuwa kubwa.

Mahundi alisema kwa kawaida mwanamke akiwa mjamzito anategemea kupata mtoto mmoja ama wawili, lakini kwa mwanamke sio la kawaida na kutakiwa kusaidiwa.

Alisema kupata watoto wanne kwa mwanamke ni furaha kubwa, lakini kiafya inaweza kuwa hatari endapo hatapata huduma bora za afya, aliwapongeza madaktari wa Hospitali ya Wilaya ya Chunya kwa huduma waliyompatia.

"Mimi kama mwanamke mwenzake nimeguswa sana na mwenzangu huyu kwa zawadi aliyoipata, sisi tumekuja kumwona, lakini tutamsaidia hata makopo kadhaa ya maziwa kwa ajili ya watoto hawa, lakini niwaombe Watanzania wengine waguswe," alisema Mahundi.

Kwa upande wake, Mbunge wa Jimbo la Lupa, Kasaka alisema atatembelea nyumbani kwa mwanamke huyo ili aone mazingira yalivyo ili atoa msaada unaostahili.

Alisema amekuwa akifuatilia taarifa za afya ya mama huyo pamoja na watoto wake na akawaomba Watanzania wamsaidie kupata bima ya afya kwa ajili yake na watoto wake.

Stella alijifungua watoto hao wiki tatu zilizopita katika Kituo cha Afya cha Chalangwa na kuhamishiwa Hospitali ya Wilaya ya Chunya kwa ajili ya uangalizi maalumu.





Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, akivishwa shada la maua na kijana Subira Juma Hassan, baada ya kuwasili kwenye Uwanja wa Ndege wa Pemba jana, kwa mara ya kwanza tokea kuteuliwa kushika wadhifa huo. **PICHA: OMPR – ZNZ**

# Wenye ulemavu watakiwa kuwa mfano bora

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdallah, amesema serikali inapenda kuona watu wenye ulemavu wanakuwa mfano bora katika uwajibikaji ndani ya taifa hasa ikizingatiwa kwamba jitihada zao wanazochukua zimelenga kujikomboa katika harakati zao za kimaisha.

Alisema hayo juzi wakati akizungumza na uongozi wa idara ya watu wenye ulemavu huko katika idara hiyo, Migombani Mjini Unguja.

Alisema watu wenye ulemavu wana nguvu na uwezo mkubwa wa kufanya kazi kama walivyo wengine kwenye uwajibikaji, lakini kinachohitajika kwa jamii inayowazunguka ni kukubali kuwapa dhamana kwa mujibu wa maarifa, elimu na vipaji walivyobarikiwa.

Hata hivyo, alisema watu hao wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ndani ya jamii hasa kudhalilishwa kijinsia na matokeo yake hubaguliwa na kudharauliwa mambo yanayokwenda kinyume na haki za binadamu.

Alisema wakati serikali ikiendelea na wajibu wake katika kuzingatia utatuzi wa changamoto za watu hao wenye mahitaji maalum, wananchi pamoja na taasisi za kijamii lazima zifikie uamuzi wa kuondoa manyanyaso hayo kwa kuwapatia fursa wanazostahiki ili nao wajihisi kuwa sehemu ya jamii.

Alisema amefarajika na mafanikio makubwa yaliyopatikana ndani ya idara ya watu wenye ulemavu na kuwashukuru watendaji kwa kazi kubwa wanazozifanya katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

Akitoa taarifa, Mkurugenzi wa Idara ya Watu Wenye Ulemavu, Abeda Rashid Abdulla, alisema watendaji wa idara hiyo wamebadilika kimfumo kuelekea katika teknolojia ya kisasa ya habari na mawasiliano yanayowapa uharaka wa kutekeleza majukumu yao.

Mkurugenzi huyo alisema mfumo huo umewawezesha watendaji wa idara hiyo kusajili watu wenye ulemavu katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba, kuanzia ngazi ya shehia jambo ambalo lilikuwa likichukuwa muda mrefu na wakati mwingine changamoto ya kuyafikia baadhi ya maeneo hasa vijijini.

Pia, Makamu wa Pili alitembelea Tume ya Taifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za kulevya Zanzibar, Kilimani na Mkurugenzi Mtendaji wa Tume hiyo, Kheriyangu Mgeni Khamis, alisema wapo vijana 3,161 waliofanikiwa kuacha kutumia dawa za kulevya hadi mwaka 2019.

Kheriyangu alisema marekebisho ya baadhi ya sheria na kanuni kwa ushirikiano wa pamoja wa kitaifa, kikanda na kimataifa ndio iliyosababisha mafanikio hayo ya kuiokoa nguvu kazi ya vijana kuendelea kutumbukia ndani ya janga la matumizi ya dawa za kulevya.

# Mfanyabiashara asaidia madawati 1,500

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ZAIDI ya madawati 1,500 yenye thamani ya Sh. milioni 240 yametolewa na mfanyabiashara, Khaled Al-khaudi kutoka nchini Abudhabi kwa lengo la kupunguza tatizo la uhaba wa madawati nchini.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, alisema upatikanaji wa madawati kutaisaidia wizara yake kuondokana na tatizo la madawati katika shule zake.

Akizungumza jana wakati alipofika kuangalia msaada huo pamoja na meza za maabara eneo la kwa Mchina, Simai alisema serikali ya awamu iliyopita imefanya kazi kubwa ya kununua madawati na zaidi ya madawati 44,000 yamenunuliwa kwa shule za sekondari na zaidi ya madawati 11,000 kwa ajili ya shule za msingi.

Alisema ana imani kuwa msaada walioupata kwa awamu ya kwanza utasaidia kupunguza tatizo la madawati na kuhakikisha watoto wote wanapata madawati.

Alisema licha ya madawati hayo pia kuna awamu nyingine itafuata huku akiwaomba wafanyabiashara na wadau wengine wanaoishi nje ya nchi kusaidia sekta ya elimu ambayo michango yao wanaithamini katika kuleta maendeleo ya elimu nchini.

Naye mratibu wa madawati hayo kutoka kwa mfadhili, Sabine Emmerich, alisema msaada huo umetolewa kwa lengo la kuwafikia zaidi wanafunzi wa Shule za Nungwi, Mkoa wa Kaskazini Unguja pamoja na shule za karibu ya mkoa huo zenye mahitaji kwa kuhakikisha walimu wanafanya kazi yao vizuri na wanafunzi nao kusoma katika mazingira mazuri.

Alisema endapo msaada huo utatumika kama ulivyokusudiwa Khaled ambaye ni mdhamini wa madawati hayo ataendelea kusaidia zaidi ili kuleta maendeleo katika elimu.

# Kuchelewa ujenzi mahakama kwamkera waziri

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, amesema hajafurahishwa na kasi ya ujenzi wa jengo la Mahakama Kuu huko Tunguu na kukerwa na visingizio vya ugonjwa wa corona na tatizo la uhaba wa mchanga katika kukamilisha miradi ya serikali.

Akizungumza jana na watendaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar, wakiongozwa na Jaji Mkuu, Omar Othman Makungu, huko Vuga, alisema haipendezi hata kidogo kuona ujenzi wa mradi wa jengo la kisasa la Mahakama Kuu, limeshindwa kukamilika katika kipindi cha uongozi wa Rais mstaafu Dk. Ali Mohamed Shein, ambaye ndiye aliyeanzisha mradi huo wenye lengo la kuhakikisha Zanzibar inakuwa na majengo ya kisasa ya mahakama.

Alisema visingizio vya makandarasi wa mradi huo ambao ulikuwa ukabidhiwe serikalini Oktoba 20, mwaka huu, havikubaliki na suala la mchanga halimo katika makubaliano ya mkandarasi na serikali.

"Nimesikitishwa na kuchelewa kukamilika kwa mradi huu ambapo visingizio vilivyotolewa na mkandarasi havikubaliki...suala la mchanga ni jukumu la mkandarasi na sio serikali wakati ugonjwa wa corona sio jambo la msingi na kuufanya mradi huo kuchelewa kukamilika kwake.

Suleiman alisema serikali imechukua uamuzi wa kujenga jengo jipya la mahakama kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kupata nafasi nzuri ya kusikiliza mashauri yao, huku watendaji ikiwamo majaji na mahakimu kusikiliza kesi kwa faragha zaidi.

Akitoa maelekezo kwa mkandarasi huyo, alisema mradi huo unakamilika mwishoni mwa mwezi wa Desemba na kufunguliwa katika Sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar.

"Namtaka mkandarasi wa mradi huu kukamilisha kazi za jengo hili ifikapo Desemba mwaka huu...lakini tunataka kazi ifanywe kwa kuzingatia viwango na ubora wake kwa ujumla," alisema.

Kwa upande wake msimamizi wa mradi wa ujenzi wa jengo la Mahakama Kuu ya Zanzibar huko Tunguu, Kai Bashiri, alitaja miongoni mwa sababu zilizosababisha mkandarasi wa mradi huo kampuni ya Advert Construction kuchelewa kukamilisha kazi kwa wakati ni kuwapo kwa tatizo kubwa la uhaba wa mchanga.

Alisema wamekuwa wakipata tani 100 za mchanga kwa wiki sawa na gari kumi kwa wiki ambazo hazitoshelezi mahitaji ya mradi huo mkubwa.

Alizitaja sababu nyingine ikiwamo kuzuka kwa ugonjwa corona ambao umesababisha baadhi ya vifaa kushindwa kuwasili nchini kwa wakati kutoka nje ya nchi.

"Baadhi ya vifaa ikiwamo madirisha ndiyo vimewasili nchini juzi...tatizo kubwa ni kuzuka kwa ugonjwa wa corona ambao bado unaendelea kuisumbua dunia hadi sasa," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**
Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:
- **Kuboresha biashara**
- **Kulipa kodi ya nyumba**
- **Kumalizia tenda**
- **Kulipa matibabu n.k.**

Mawasiliano yetu:
**Dar es salaam – 0768 928 516.**
**Arusha – 0677 226 960.**

## NAFASI ZA MASOMO


**KELAND NURSERY AND PRIMARY SCHOOL** ILIYOPO SALASALA RTD INATANGAZA NAFASI ZA AWALI NA MSINGI. KWA MAWASILIANO **PIGA SIMU: 0713 327613.**


## NIPASHE NI JIBU LAKO

**NJOO UTANGAZE NASI**
**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**ELVIS EXAVERY VICENT** anatangaza kupotelewa kwa result slip ya kidato cha nne yenye index namba **S1722/0215/2019** iliyotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary TEMEKE mwaka 2019,yeyote atakayeikota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **DAR/CHA/RB/821701/2020**

116016402

## TANGAZO LA KUPOTEA OFA YA KIWANJA

**Edwin Sifael Moshi**
Anatangaza kupotelewa na Ofa ya kiwanja namba **45 Kitalu "DD" (HD)** Ngokolo Manispaa ya Shinyanga. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Edwin Sifael Moshi kwa simu namba **0713-472252**
RB namba: **SHY/RB/2020.** Control namba **9910819625821**

JACOB F./MWINUKA
AFISA ARDHI
MANISPAA SHINYANGA

AFISA ARDHI WA MANISPAA SHINYANGA

116015002

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
ILIYOPO MOROGORO

TANGAZO LA KUITWA SHAURINI

SHAURI LA MADAI/TARAKA/MIRATHI; NAMBA:87..2020

Mdai: THEOPISTA PIUS MKUNJA
DHIDI YA
Mdaiwa: LUVINUS FIDELIS MCHANDE

Kwa: LUVINUS FIDELIS MCHANDE
WA JWTZ, KIGOMA

Ombi la Mdai: THEOPISTA PIUS MKUNJA

Madai ya: TARAKA,MGAWANYO WA MALI

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 07 mwezi 12 mwaka 2020 saa 02:30 Asubuhi/alasiri.
Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 26 mwezi 11 mwaka 2020.

Anaomba tangazo lake litolewe kesho kwenye gazeti la nipashe.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO.

116015902

KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA

SHAURI LA ARDHI RUFAA NO.4 OF 2020

PROSPER EVARISTO SANGA.......................MRUFANI

DHIDI YA

1. SINA WILSON WALONDE.......................MRUFANIA
   @UPENDO WALONDE
2. JOB MWINUKA.......................................MRUFANIA
3. CHRISTOPHER KINYUNU.......................MRUFANIA
4. YONO AUCTION MART & CO.LTD............MRUFANIA

KWA : CHRISTOPHER KINYUNU,
POPOTE ULIPO.

**KUITWA SHAURINI**

Unaamriwa na mahakama hii uhudhurie hapa mahakama kuu Kanda ya Mbeya tarehe 18/02/2021 siku ya Alhamisi saa 3:00 asubuhi ambapo shauri limepangwa kusikilizwa.
Elewa kwamba,ukikosa kufika siku hiyo shauri hilo litasikilizwa upande mmoja bila wewe kuwepo na uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa mahakama leo hii tarehe 23 Mwezi Novemba,2020.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA

116016102

## TANGAZO LA KUPOTEA HATI MILIKI YA NYUMBA.

**LIBORI MELKIAD ERRO.**
Anatangaza kupotelewa na hati miliki ya nyumba ya makazi ya muda, yenye namba **244 BLOCK J.**
Iliyotolewa na Halmashauri ya Wilaya ya KARATU.
Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu.
Taarifa ya polisi :-
**KRT/RB/1862/2018.**

116015802

## KUPOTEA KWA VYETI



**JULIANA JOSEPH NELSON** anatangaza kupotelewa na cheti che kidato cha nne chenye index namba **S.1855/0008** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia Butiama Sekondari mwaka 2017 pamoja na Result Slip yake. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.281/0597** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia Chief Ihunyo Girls High School mwaka 2020 pamoja na Result Slip yake. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **MS/RB/6347/2020.**

116014902


**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI**

**INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042,**

**DAR ES SALAAM.**

**MOB:**

**+255 - 0782253676**

***Uza,***

***Chenye Thamani Kubwa Kwa***

***Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***


JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA

### TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu mwananchi mnatangaziwa tarehe 27/11/2020 kampuni ya **chico (china henan internation cooperation group co.ltd) itasafirisha mzigo (Concrete Pillar)** wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DODOMA** kuelekea **TABORA kupitia ITIGI,** gari hilo lenye namba za usajiri **T507 BKM / T509 BKM, yenye escort no T643 CVZ**
2. Gari hilo linavipimo vifuatavyo
   **Urefu - mita 20.00m**
   **Upana - 3.00m**
   **Kimo - 4.5m**
3. Njia itakayo tumika ni **DODOMA hadi TABORA kupitia ITIGI** Gari itasafiri muda wa mchana tu kuanzia saa 12:30 asubuhi mpaka saa 12:00 jion

116015402

***Tunaomba radhi kwa usumbufu***

JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA

### TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu mwananchi mnatangaziwa tarehe 04/12/2020 kampuni ya **chico (china henan internation cooperation group co.ltd ) itasafirisha mzigo (Greader)** wake wenye vipimo vikubwa kutoka **TABORA kuelekea DODOMA kupitia ITIGI,** gari hilo lenye namba za usajiri **T507 BKM / T509 BKM, yenye escort no T643 CVZ** Gari hilo linavipimo vifuatavyo
   **Urefu - mita 20.00m**
   **Upana - 3.00m**
   **Kimo - 4.5m**
2. Njia itakayo tumika ni **TABORA** hadi **DODOMA** kupitia ITIGI
3. Gari itasafiri muda wa mchana tu kuanzia saa **12:30 asubuhi mpaka saa 12:00 jioni**

116015402

***Tunaomba radhi kwa usumbufu***


**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Waziri Mkuu Ethiopia aamuru mashambulio dhidi ya mji wa Mekele

**Addis Ababa, Ethiopia**

WAZIRI Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, amesema ameanzisha awamu ya mwisho ya operesheni ya kijeshi katika jimbo la Tigray, kuanza kushambulia mji mkuu wa jimbo hilo, Mekelle.

Amesema wanajeshi watajaribu kutowajeruhi raia na kutoa wito kwa watu katika mji huo kusalia majumbani mwao.

Hatua hiyo inakuja baada ya muda wa mwisho, uliotolewa kwa wapiganaji wa Tigray kujisalimisha, kumalizika siku ya juzi.

Chama cha TPLF, ambacho kinadhibiti mji wa Mekelle, kimeapa kuendelea na mapigano.

Mamia ya watu wameripotiwa kuuawa na maelfu ya wengine kutoroka kwao, huku vikosi vya muungano vya Ethiopia, vikiteka miji kadhaa ya Tigray kutoka kwa wapiganaji wa TPLF.

Hata hivyo imekuwa vigumu kupata maelezo kuhusu mapigano hayo, kutokana na mawasiliano ya simu na huduma za intaneti katika jimbo la Tigray, kukatizwa .

Mwaka jana. Abiy alivunja muungano tawala, unaojumuisha vyama vilivyoundwa kwa misingi ya kikabila, na kuviunganisha katika chama kimoja, national party, the Prosperity Party, ambacho TPLF walikataa kujiunga.

Utawala wa Tigray, unayaona mageuzi ya Abiy, kama jaribio la kujenga mfumo serikali moja na kuharibu mfumo uliopo sasa wa shirikisho.

Pia hukasirishwa na kile inachokiita urafiki wa waziri mkuu na rais wa Eritrea Isaias Afwerki usiokuwa na kanuni .

Abiy, ambaye ni mshindi wa tuzo ya amani ya Nobel, mwaka 2019 kutokana na juhudi zake za kuleta amani kwa kumaliza mzozo wa muda mrefu wa nchi yake na Eritrea.

Kwa upande wake, anaamini kuwa maofisa wa TPLF wanahujumu mamlaka yake.

Aliamuru mashambulio ya kijeshi dhidi ya TPLF baada ya kusema kuwa wapiganaji wake walikuwa wamevuka mstari wa mwisho mwekundu, akiwashutumu kwa kushambulia kambi ya kijeshi ya vikosi vya shirikisho Novemba 4, mwaka huu.

*BBC*




Maofisa usalama wakiwa sehemu ambayo miili ya watu 103 imegundulika kwenye kaburi la halaiki lililofukuliwa katika uwanja wa El Salto ulioko Jalisco, nchini Mexico. **PICHA/TRT**

# Trump asema uchaguzi wa Marekani ulijaa ufisadi

**Washington, Marekani**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amesema kuwa yeye ndiye mshindi wa kweli wa uchaguzi wa urais wa Novemba 3, mwaka huu.

"Tunapaswa kurudisha uchaguzi huu nyuma. Tunachohitaji ni majaji ambao wanatusikiliza vizuri.

Trump alitoa matamko hayo kwa njia ya simu katika kikao kilichofanyika juu ya madai ya kasoro za uchaguzi katika bunge la jimbo la Pennsylvania.

"Hatukutendewa haki katika majimbo yote muhimu. Katika uchaguzi huu, kulikuwa na ufisadi mwingi."

Alisisitiza kuwa mchakato wa uchaguzi bado haujaisha, ikiwa kura zinazotumiwa kisheria zitahesabiwa, itafichuliwa kuwa wao ndio washindi.

"Wanademokrat walipoteza uchaguzi huu. Walidanganya katika uchaguzi." aliongeza Rais Trump.

"Tunapaswa kurudisha uchaguzi huu nyuma. Tunachohitaji ni majaji ambao watatusikiliza vizuri."

*TRT*

# Mgonjwa wa kwanza kupasuliwa ubongo akiwa macho

**Nairobi, Kenya**

NCHINI Kenya, umefanyika upasuaji wa kwanza wa ubongo, huku mgonjwa akiwa macho.

Upasuaji huo umefanyika katika Hospitali ya Nairobi, huku mgonjwa huyo akiwa macho na kuzungumza wakati wote.

Madaktari wa upasuaji wanategemea mchakato huo wakipekee ambao bado ni wa hatari kuleta matokeo bora na kupunguza hatari ya jeraha katika ubongo.

Madaktari bingwa wa upasuaji wa fuvu la kichwa pia walifuatilia hali ya mgonjwa wakati wote wa upasuaji, ikimaanisha kuwa wanaweza kuondoa uvimbe ambao kwa kawaida usingeweza kutolewa salama.

Upasuaji huo wa kufungua fuvu la kichwa 'brain craniotomy', unaangaliwa kama mafanikio makubwa katika sekta ya tiba nchini humo.

*BBC*

# Mradi wa IFAD waepusha vifo watoto wa kike

**New Delhi, India**

MFUKO wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (IFAD), umesaidia wakazi wa eneo la Maharashtra, nchini India, kuondokana na tabia utoaji mimba za watoto wa kike.

Msaada huo ni harakati za kukabiliana na ukatili dhidi ya wanawake, nchini India.

Mradi umesaidia zaidi ya wanawake milioni moja kwa kuwajengea uwezo kifedha na kitamaduni.

Licha ya sheria za kupiga marufuku uchunguzi wa ujauzito, ili kuepusha utoaji mimba za watoto wa kike, bado sehemu nyingi nchini India kuwa na mtoto wa kike inaonekana ni jambo la kukatisha tamaa.

Mradi huo unahamasisha jamii kuona watoto wa kike sawa na wa kiume

IFAD inasema juhudi za pamoja kupitia mradi kama huo, zimeleta mafanikio makubwa na kuongeza idadi ya watoto wa kike wanaozaliwa.

Nchini humo, wanawake wa jamii ya Maharashra wamekuwa wakigonga kifaa maalum kuashiria tukio maalum la sherehe ambalo ni uzao wa mtoto.

Awali sherehe kama hizo, zilikuwa ni za uzao wa mtoto wa kiume na si wa kike, kwa kuwa mtoto wa kike hakupewa kipaumbele.

*UN*

# Kaburi la halaiki lapatikana Mexico

**Jalsico, Mexico**

MIILI ya watu 103 imegundulika kwenye kaburi la halaiki lililofukuliwa nchini Mexico.

Kulingana na taarifa iliyochapishwa na vyombo vya habari vya nchini humo, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali, miili 103 iligunduliwa kwenye kaburi la halaiki wakati wa shughuli ya utafutaji iliyofanyika katika uwanja wa El Salto ulioko Jalisco.

Katika ukaguzi wa kwanza, watu 30 wakiwamo wanawake wawili walitambuliwa na familia zao.

Ripoti iliyochapishwa Oktoba, mwaka huu, na Tume ya Kitaifa ya Utafutaji ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Mexico, ilisema kuwa miili 897 ilipatikana katika makaburi ya siri yaliyogundulika wakati wa ukaguzi huko Jalisco kati ya mwaka 2006 na mwaka 2010 huu

Kwa upande mwingine, katika ukaguzi uliofanywa mwaka 2006 nchini humo, jumla ya miili ya watu 6,900 ilipatikana kwenye makaburi 4,092 ya siri yaliyofukuliwa.

*TRT*

**Katika ukaguzi wa kwanza, watu 30 wakiwamo wanawake wawili walitambuliwa na familia zao.**



# DIEGO ARMANDO MARADONA

## GWIJI ALIYEACHA ALAMA ISIYOFUTIKA KWENYE SOKA

**BUENOS AIRES, Argentina**

DIEGO Armando Maradona mmoja wa wachezaji waliobarikiwa, Argentina ilijivunia kipaji cha kipekee, madoido ya ajabu akiwa uwanjani, maono na kasi iliyovutia mashabiki wengi.

Lakini alisababisha hasira na goli lake alilolipa jina 'Hand of God' (Goli la mkono wa Mungu) ambalo lilizua utata pamoja na kutumbukia katika utumiaji wa dawa za kulevya na mapungufu mengine yaliyojitokeza baada ya kustaafu soka.

**ALIKOTOKA**

Alizaliwa Oktoba 30, mwaka 1960 katika kitongoji duni cha Lanús jijini Buenos Aires nchini Argentina.

Aliepukana na umaskini wakati akiwa kijana kwa kuwa nyota wa mpira wa miguu ambaye kuna wale wanaomchukulia kuwa bora zaidi akilinganishwa na mchezaji Pele wa Brazil.

Maradona aliyefunga magoli 259 katika mechi 491 alizoshiriki, alimshinda Pele ambaye ndio mpinzani wake mkuu wa soka kwa bara la Latin Amerika katika kura ya maoni ya kuamua mchezaji bora wa karne ya 20, kabla ya Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), kubadilisha sheria za upigaji kura na wote wawili wakatunukiwa hadhi hiyo.

Maradona alionyesha uwezo wa hali ya juu kutoka akiwa mtoto na kuwa chanzo cha timu ya vijana ya Los Cebollitas kuwa kidedea kwa kupata magoli 136 bila kufungwa na timu yoyote, na akawa mchezaji wa kimataifa akiwa na umri wa miaka 16 na siku 120 tu.

Akiwa mfupi wa futi tano na inchi tano pekee, uchezaji wake haukuwa wa kawaida.

Lakini ujuzi wake, wepesi, maono, jinsi alivyodhibiti mpira, alivyopiga chenga na kupitisha mpira kwa wengine lilikuwa jambo la ajabu zaidi.

Huenda alikuwa na kasi ya ajabu mno akiwa uwanjani karibu na mahasimu wake, lakini alikuwa na wakati mgumu kukwepa changamoto.

**'GOLI LA MKONO WA MUNGU'**

Yeye ndio chanzo cha nchi yake kuibuka na ushindi kwenye fainali za Kombe la Dunia mwaka 1986 nchini Mexico na kupata fursa kuingia fainali miaka minne baadaye.

Katika robo fainali ya mchezo wa awali kulijitokeza utata ambao kumbe baadaye ukaja kukumbukwa katika maisha yake yote.

Mechi dhidi ya England ilikuwa na mkwaruzano uliopitiliza kidogo, huku vita vya zamani za kugombea maeneo ya utawala wa Visiwa vya Falklands kati ya nchi hizo mbili ikiwa ndio imetokea miaka minne tu nyuma. Na hilo likasababisha hali uwanjani kuzua wasiwasi zaidi.

Dakika 51 zikiwa zimekatika na hakuna timu iliyoona lango la mwingine, Maradona aliruka na mlinda mlango wa England, Peter Shilton na kufunga kwa kupiga mpira kwa mkono na ukuja wavuni.

Licha ya England kulalamika kwamba, mpira ule ulipigwa kwa mkono na sio kichwa, lakini Argentina walipewa bao hilo na kuzua vurugu uwanjani hapo.

Dakika nne baadaye, alifunga bao ambalo linakumbukwa kama 'goli bora la karne' - baada ya kuchukua mpira mwenyewe na kuanza mbio kwa kasi ya ajabu kutoka nyuma ya uwanja na kuwapiga chenga wachezaji karibia nane na akamzunguka golikipa Shilton na kufunga bao.

"Lazima tu ungesema ulikuwa mchezo mzuri. Hakuna shaka yoyote na goli hilo. Kulikuwa tu na mchezaji nyota wa mpira wa soka," alisema mchambuzi wa BBC Barry Davies.

England ilikuwa nyuma kwa bao moja, lakini Argentina ikafaulu na Maradona akasema "ilikuwa zaidi ya kushinda mechi, ilikuwa ni suala na kuwatoa nje Waingereza".

**SHUJAA WA NAPOLI**

Maradona alivunja rekodi ya uhamisho mara mbili, wakati akiondoka kutoka timu ya vijana ya Boca Juniors kujiunga na Barcelona ya Hispania kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni tatu mwaka 1982.

Pia akavunja rekodi ya pili wakati akitoka Barcelona kwenda Napoli ya Italia kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni milioni tano, miaka miwili baadaye.

Waliomlaki walikuwa ni mashabiki zaidi ya 80,000 waliomsubiri kwenye Uwanja wa San Paolo alipowasili kwa helikopta.

Alichezea klabu bora nchini Italia akishangiliwa na wafuasi wake wakati huo akiwa kichocheo cha kupata mataji ya mawili ya Ligi Kuu mwaka 1987 na 1990 na pia katika Kombe la Uefa mwaka 1989.

Sherehe ya kufurahia ushindi wa kwanza ilidumu kwa siku tano huku mamia ya maelfu ya watu wakijitokeza, lakini Maradona alionekana kuchoshwa na sherehe hizo.

"Huu ni mji mzuri, lakini napata shida, hata siwezi kupumua kwa amani. Nataka kuwa huru na kutembea. Mimi ni kijana kama mwingine yeyote yule," alisema.

Hata hivyo, hakuweza kujitenga na sakata ya uhalifu na akatumbukia katika utumiaji wa dawa za kulevya na kufunguliwa kesi mahakamani.

Baada ya kufungwa bao 1-0 na Ujerumani mwaka wake wa mwisho nchini Italia mwaka 1990 kwenye Kombe la Dunia, alipatikana na kashfa ya utumiaji wa dawa zilizopigwa marufuku mwaka uliofuata na kupigwa marafuku kucheza soka kwa miezi 15.

Hata hivyo, alirejea tena kwenye ulimwengu wa soka katika Kombe la Dunia la mwaka 1994 nchni Marekani.

Lakini pia alifanya watazamaji kuwa na wasiwasi jinsi alivyosherehekea goli akiwa kama kichaa mbele ya kamera na kutolewa nje katikati ya mechi baada ya kubainika kuwa ametumia dawa iliyopigwa marufuku ya ephedrine.

**KUSTAAFU**

Baada ya kupatikana tena ametumia dawa zilizopigwa marufuku, miaka mitatu baadaye alistaafu kucheza soka akiwa na umri wa miaka 37, lakini akaendelea kuandamwa na matatizo.

Maradona alihukumiwa kifungo cha miaka miwili na miezi 10 kilichocheleweshwa kwa sababu ya kuwafyatulia risasi wanahabari.

Tabia yake ya kutumia dawa za kulevya na pombe ilimsababishia matatizo mengi ya kiafya.

Aliongeza uzito na kuna wakati fulani alikuwa na kilo 128.

Mwaka 2004 akapata mshtuko wa moyo uliosababisha apelekwe katika chumba cha wagonjwa mahututi.

Pia alifanyiwa upasuaji wa kupunguza tumbo lake kumsaidia kukabiliana na tatizo la uzito wa kupindukia na kutafuta hifadhi nchini Cuba wakati anakabiliana na utumiaji wa dawa za kulevya.

MATUKIO

1977: Alijitokeza katika mchuano kati ya Argentina vs Hungary.

1982: Alijiunga na Napoli baada ya kuwa Barcelona kwa miaka miwili ya mafanikio makubwa.

1986: Alishinda Kombe la Dunia akichezea Argentina.

1990: Alikuwa mshindi wa pili wa Kombe la Dunia akichezea Argentina.

1991: Alisimamishwa kucheza soka kwa muda wa miezi 15 baada ya kuthibitishwa kutumia dawa zilizopigwa marufuku.

1994: Alicheza katika Kombe la Dunia kwa mara ya nne, lakini akatolewa nje baada ya kuthibitishwa kutumia dawa zilizopigwa marufuku.

1997: Alistaafu kucheza soka baada ya kuthibitishwa kutumia dawa zilizopigwa marufuku kwa mara ya tatu.

2010: Alikamilisha miaka miwili ya kuwa Kocha wa Argentina baada ya kutolewa katika robo fainali ya Kombe la Dunia nchini Afrika Kusini.

HABARI MICHEZO




# MESSI, RONALDO WAMLILIA MARADONA

**BARCELONA, Hispania**

DIEGO Maradona amepigiwa saluti na Lionel Messi na Cristiano Ronaldo kama "ajabu lisilofutika" kwenye soka baada ya gwiji huyo wa soka kufariki dunia akiwa na umri wa miaka 60.

Messi, nyota wa kizazi cha sasa cha soka wa Argentina ambaye amefuata nyayo za gwiji huyo kwa kucheza pale Barcelona na timu ya taifa, aliweka picha kwenye ukurasa wake wa Instagram waliyokumbatiana na Maradona huku wakitabasamu.

Aliandika: "Ni siku ya huzuni sana kwa Waargentina wote na mpira wa miguu. Ametuacha sisi, lakini hajatuacha moja kwa moja, kwa sababu Diego yupo ndani yetu.

"Daima nitakukumbuka nyakati zote nzuri nilizokuwa na yeye na nataka kutuma salamu za rambirambi kwa marafiki zake wote pamoja na familia yake. RIP."

Kwa upande wake, Ronaldo aliweka picha ya yeye na Maradona kwenye ukurasa wake wa Instagram na kuandika: "Leo nasema kwaheri kwa rafiki na dunia inasema kwa heri kwa gwiji wa soka.

# UWANJA WA NAPOLI KUITWA MARADONA

**NAPLES, Italia**

RAIS wa Napoli, Aurelio De Laurentiis, amebainisha kwamba, klabu inafanya mchakato wa kubadilisha jina la uwanja wao na kumpa heshima Diego Maradona baada ya kifo chake Jumatano.

Maradona, ambaye bila shaka yoyote ni mmoja wa wachezaji bora zaidi wa soka kuwania kutokea duniani, alifariki dunia juzi akiwa na umri wa miaka 60 kwa mshtuko wa moyo, Chama cha Soka cha Argentina (AFA), kilithibitisha Jumatano.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia akiwa na Argentina, Maradona alifurahia mafanikio makubwa zaidi kwenye soka akiwa mjini Naples, ambako aliiongoza Napoli kutwaa taji la Ligi Kuu Italia, Serie A, msimu wa 1986-87 na 1989-90 - ambapo ndio wakati pekee klabu hiyo imewahi kulitwaa taji hilo mara mbili na haijafanikiwa tena hadi leo.

Mashabiki wa Napoli walijaa katika mitaa ya mji wa Naples wakiombeleza kifo cha Maradona - na De Laurentiis akasema Uwanja wao wa San Paolo unaweza kubadilishwa jina na kupewa Maradona.

"Linaweza kuwa wazo zuri kuubadilisha jina la Uwanja wa San Paolo na kuuita Maradona, ni kitu ambacho tunakifikiria," alisema De Laurentiis akinukuliwa na RMC Sport.

Naye Meya wa Jiji la Naples, Luigi de Magistris, pia aliandika kupitia ukurasa wake wa Twitter: "Tuubadilishe jina uwanja wa San Paolo na kuuita Diego Armando Maradona!!!"



## FIFA YATAKIWA KUIONDOA NAMBA 10 YA MARADONA

**PARIS, Ufaransa**

KOCHA Mkuu wa Marseille, Andre Villas-Boas, amelishauri Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), "kuiondoa jezi namba 10 kwenye mashindano yote ya soka" ili kutoa heshima kwa Diego Maradona.

Maradona, ambaye anatajwa kama mmoja wa wachezaji bora zaidi wa wakati wote, alifariki dunia akiwa na umri wa miaka 60, Jumatano kwa mshtuko wa moyo.

Alitamba na jezi namba 10 akiwa na Napoli na Argentina kipindi chake chote cha uchezaji, na namba hiyo ya jezi ilistaafishwa na klabu hiyo ya Serie A mwaka 2000 kwa ajili ya heshima yake.

Na sasa Villas-Boas anataka FIFA kuifuta moja kwa moja jezi namba 10 kutotumika kwenye mashindano yoyote ya soka duniani.

"Kwa Maradona, ni pigo kubwa. Ningependa FIFA kuiondoa jezi namba 10 kwenye mashindano yote na kwa timu zote," alisema akiwaambia waandishi wa habari baada ya Marseille kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya FC Porto kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Jumatano.

"Nafikiri njia bora ya kutoa heshima kwa wachezaji wakubwa katika historia ya soka ni kustaafisha namba ya jezi walizotumia."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# KLOOP ALIA NA RATIBA YA EPL

Kocha huyo aeleza ratiba hiyo waliyopangiwa Liverpool ni kama 'uhalifu' huku wakiwa wameshindwa...

**LIVERPOOL, England**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, ameiita ratiba ya timu yake ni "uhalifu" wakati akijiandaa kuivaa Brighton and Hove Albion kwenye mechi ya Ligi Kuu England ndani ya siku tatu, baada ya kuchezea kichapo cha 2-0 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kutoka kwa Atalanta.

Mabao ya kipindi cha pili kutoka kwa Josip Illicic na Robin Gosens yaliwasaidia miamba wa Ligi Kuu Italia, Serie A, Atalanta kupata ushindi usiotarajiwa kwenye mchezo huo wakiwa ugenini.

Liverpool ilitoka kuwafumua mabao 5-0 wiki tatu zilizopita kwenye michuano hiyo ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na sasa wekundu hao wa Anfield wameshindwa kufuzu hatua ya mtoano hadi mechi zijazo.

Matokeo hayo ya Jumatano yaliwaacha mabingwa hao wa Ligi Kuu England wakiwa wameshinda mechi moja kati ya tatu zilizopita wakati wakikaribia kufikisha mechi nne za kucheza ndani ya siku 12.

Klopp alitabiri kwamba sio wachezaji wake pekee ambao wanakabiliwa na rartiba hiyo ngumu akiiambia BT Sport: "Ninahofu kusema nafikiri inaweza kuwa sio sisi tu, pengine timu nyingine nazo zinakabiliwa na wakati huu mgumu.

"Tunatakiwa kucheza mechi Jumamosi saa 12:30 (saa 9:30 kwa Bongo), kitu ambacho ni sawa na uhalifu.

"Kwa sasa sina cha kufanya kuhusu mchezo wetu tuliopoteza usiku huu (juzi).

"Kwa sasa natakiwa kushukuru, sina mchezaji ambaye ameumia. Tunatakiwa kuacha haraka kuifikiria mechi iliyopita na kuangalia inayokuja mbele yetu.

Katika mchezo huo, kikosi hicho cha Klopp kilikuwa na wakati mgumu kupenya ngome ya lango la Atalanta."

Liverpool ilipiga shuti moja tu lililolenga goli likipigwa na Mohamed Salah katika dakika ya 44.

Ikiwa ni kwa mara ya kwanza kwa Liverpool kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu msimu wa 2003-04, ikiwa inacheza katika dimba la nyumbani.

## KWA UFUPI

**ERIKSEN ANUKIA ARSENAL**

ARSENAL imepewa fursa ya kumsajili kiungo wa kati wa Inter Milan, Christian Eriksen katika makubaliano ya bei ya chini, ikiwa ni miezi 10 baada ya raia huyo wa Denmark mwenye umri wa miaka 28, kuondoka Tottenham Hotspur. ***(ESPN)***

**GIROUD AKARIBIA INTER**

KLABU ya Inter Milan itajaribu kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Olivier Giroud mwenye umri wa miaka 34 kutoka Chelsea wakati wa dirisha dogo la usajili Januari. ***(Calciomercato)***

**SZOBOSZLAI AGOMBEWA**

ARSENAL inafikiria kumsajili kiungo wa kati wa Hungary, Dominik Szoboszlai kutoka Red Bull Salzburg na kumtoa kwa mkopo kwa klabu hiyo ya Austria, kwa lengo la kuipiku RB Leipzig ya Ujerumani kutomsajili kiungo huyo. ***(Football Insider)***

**SPURS KUIBOMOA EVERTON**

KLABU ya Everton inawafuatilia wachezaji watatu wa Tottenham Hotspur kabla ya dirisha la uhamisho la Januari, ambao ni kipa Paulo Gazzaniga mwenye umri wa miaka 28, kiungo wa kati Delle Ali na Harry Winks wote wakiwa na umri wa miaka 24. ***(Football Insider)***

**SALIBA NJIA MOJA**

MLINZI wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, William Saliba mwenye umri wa miaka 19, yuko tayari kuacha mshahara wa pauni 90,000 kwa wiki ili kupata uhamisho wa mkopo kutoka Arsenal ifikapo Januari. ***(Mirror)***

**RICE AINGIA SOKONI**

KIUNGO wa kati wa West Ham United na England, Declan Rice mwenye umri wa miaka 21, amesema ni muhimu kushinda mataji licha ya uvumi kuhusu ombi la kutaka kumsajili kutoka Chelsea wakati wa dirisha la Januari. ***(Metro)***

**WILSHERE KUREJEA ARSENAL**

NYOTA wa zamani wa Timu ya Taifa ya England, Jack Wilshere mwenye umri wa miaka 28, amesema itakuwa ni ndoto yake kujiunga tena na Arsenal. ***(Sun)***

**SHEFFIELD KUMSAJILI MUSA**

KLABU ya Sheffield Wednesday inajiandaa kumnunua aliyekuwa mchezaji wa Leicester City na Nigeria, Ahmed Musa, huku mchezaji huyo ambaye yuko huru baada ya kuachiwa na klabu ya Al Nassr. ***(Football Insider)***

**CAMAVINGA, WAKALA KIMENUKA**

HATUA ya Klabu ya Real Madrid kumlenga Eduardo Camavinga imezua vita miongoni mwa mawakala, huku mchezaji huyo wa Rennes na Ufaransa mwenye umri wa miaka, 18 akivunja uhusiano na wakala wake. ***(AS - in Spanish)***

**RAIOLA ALIANZISHA ULAYA**

WAKALA maarufu, Mino Raiola amesema wachezaji 300 huenda wakajiunga na Zlatan Ibrahimovic na Gareth Bale na kuishtaki kampuni ya michezo ya EA Sports kwa kutumia watu kama wao katika michezo 'station' bila kibali. ***(Telegraph)***

**REYNOLDS AKARIBIA JUVE**

JUVENTUS imeanza kuangalia uwezekano wa kumsajili beki wa FC Dallas Mmarekani, Bryan Reynolds, ambaye ana umri wa miaka 19.***(3rd Degree)***

HABARI MICHEZO

# WASHIRIKI KILI MARATHON WAKUMBUSHWA KUJISAJILI

**Na Mwandishi Wetu**

WANARIADHA wanaotarajiwa kushiriki katika mbio maarufu za Kilimanjaro Marathon zitakazofanyika baadaye mwakani wametakiwa kukamilisha mchakato wa usajili wao kwa njia ya mtandao au Tigo Pesa, imeelezwa.

Waandaaji wa mbio hizo wamesema ni zaidi ya mwezi mmoja tangu mbio hizo zifunguliwe rasmi na tayari kuna idadi kubwa ya watu waliojisajili huku wakiwataka washiriki ambao bado hawajakamilisha mchakato huo kufanya hivyo ili kuepuka usumbufu dakika za mwisho.

Mkurugenzi wa mbio hizo, John Bayo alisema usaili unaendelea kwa njia ya mtandao- www.kilimanjaromarathon.com na Tigo Pesa kwa kubonyeza *149*20# na kufuata maelekezo na kuongeza kuwa kama miaka yote na kueleza ikifika idadi wanayoitaka watafunga mchakato huo kwa mbio zote tatu za Kilimanjaro Marathon (kilomita 42), Tigo Kili Half Marathon (kilomita 21) na Grand Malt (kilomita tano).

Bayo alisema wanazingatia idadi maalumu ili kuendana na taratibu za Shirikisho la Kimataifa la Riadha (IAAF) kwa ajili ya kuhakikisha usalama wa washiriki na upatikanaji wa huduma muhimu na pia kuhakikisha taratibu zote zinafuatwa ili kujikinga na virusi vya Covid-19.

"Tunatoa wito kwa washiriki wote wajisajili kwa wakati na kuhakikisha wanalipia ili wathibitishe ushiriki wao," alisema Bayo.

Aliongeza wanatarajia kutangaza vituo na tarehe za ugawaji namba za kukimbilia na kwa sasa washiriki waendelee kutunza ujumbe waliopokea baada ya kukamilisha malipo ya kujiandikisha.

Meneja wa Bia ya Kilimanajro na Grand Malt, Irene Mutiganzi, alitoa wito kwa washiriki wa mbio za kilomita 42 kujisajili kwa wakati kabla namba hazijaisha.

"Tunatoa wito kwa washiriki wajisajili mapema waepukane na usajili wa dakika za mwisho ili kutoa nafasi kwa waandaaji kukamilisha maandalizi," Mutiganzi alisema.

Mkuu wa Huduma za Masoko wa Tigo, William Mpinga, alisema usajili kwa Tigo Pesa umefanya zoezi hili liwe rahisi na ambao hawana laini za Tigo wanaweza kuwaomba wenzao wenye laini hizo kuwafanyia usajili.

"Natoa wito kwa washiriki wa Tigo Kili Half Marathon wajisajili kwa kubonyeza *149*20# na kufuata maelezo na kisha kukamilisha usajili wao kwa kulipia kupitia Tigopesa kwa kuwa ni rahisi na salama," alisema Shisael.

Wadhamini wa mbio hizo zitakazofanyika Februari 28, mwakani ni pamoja na Kinywaji cha Kilimanjaro, Tigo, Grand Malt, Maji ya Kilimanjaro, TPC, Simba Cement, benki ya Absa Tanzania, Unilever, hoteli ya Keys, Garda World Security, Kibo Palace na CMC Automobiles.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Aboubakar Kunenge (kushoto), akiteta jambo na msanii wa muziki wa kizazi kipya, Harmonize wakati alipotembelea studio ya msanii huyo iliyoko chini ya lebo ya Kondegang hapo jana. **PICHA: MTANDAO**

# Dube apelekwa Sauzi kutibiwa

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Azam FC, Prince Dube anatarajiwa kuondoka nchini Jumapili na kuelekea jijini Cape Town, Afrika Kusini kwa ajili ya kupatiwa matibabu baada ya kuumika mkono katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Yanga iliyochezwa juzi usiku.

Dube hakuweza kumaliza mchezo huo na alifanyiwa mabadiliko dakika 24 baada ya kuumia mkono na nafasi yake kuchukuliwa na Richard Djod, katika mchezo huo uliochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi na kumalizika kwa wageni Yanga kushinda bao 1-0.

Akizungumza na Nipashe jana, daktari msaidizi wa Azam FC, Twalib Omar, alisema uamuzi wa kumpeleka mshambuliaji huyo Afrika Kusini umekuja baada ya picha ya X-Ray kuonyesha amevunjika eneo la mkono na klabu inahitaji mshambuliaji huyo kupata matibabu sahihi.

Twalib alisema Dube anaendelea vizuri baada ya kupatiwa matibabu ya awali na wanaamini atakapokwenda Afrika Kusini, atapata huduma itakayomsaidia kupona haraka na kurejea kwenye majukumu yake kama kawaida.

"Tunatarajia kuondoka kati ya siku mbili hizi, kwenda Afrika Kusini katika hospitali ambayo wachezaji wetu huwa wanatibiwa, suala la muda gani kukaa nje ni baada ya kupata matibabu huko ndio tutafahamu zaidi," alisema daktari huyo.

Baada ya mechi hiyo, Azam yenye pointi 25 ilishushwa kileleni na Yanga iliyofikisha pointi 28 ilikaa kwenye uongozi wa msimamo wa ligi ikifuatiwa na mabingwa watetezi, Simba wenye pointi 23.

## Mgunda: Coastal tunahitaji punda

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuichapa Ihefu FC bao 1-0 katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa juzi, Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda amesema amefurahishwa na ushindi huo licha ya kwamba umekuwa finyu.

Mgunda aliliambia gazeti hili baada ya kuchapwa mabao 7-0 na mabingwa watetezi wa ligi hiyo, Simba, mashabiki wengi walitarajia wao pia wangepata ushindi mnono wa mabao dhidi ya Ihefu ambayo inaonekana ni dhaifu na vile vile kupunguza machungu.

"Coastal tunataka punda, hatutaki mlio, maana yake ni kwamba punda anabeba mzigo, kwa hiyo kama analia au halii, lakini kinachotakiwa abebe mzigo, mlio hausaidii chochote kwa sasa. Coastal kwa sasa tunahitaji zaidi pointi tatu kuliko idadi kubwa ya magoli, mashabiki wa soka waelewe hivyo," Mgunda alisema.

Kwa matokeo hayo, Coastal imefikisha pointi 15 baada ya kucheza mechi 12 na katika msimamo wa ligi iko katika nafasi ya 11 wakati vinara ni Yanga na mabingwa watetezi ni Wekundu wa Msimbazi, Simba.

## Kumekucha fainali Safari Nyama Choma

**Na Mwandishi Wetu**

FAINALI ya shindano la Safari Lager Nyama Choma linatarajia kuhitimishwa keshokutwa kwenye baa ya Govonors Pub, tukio ambalo litasindikizwa na burudani mbalimbali.

Meneja wa bia ya Safari, Pamela Kikuli, alisema jana kuwa baa 60 kutoka sehemu mbalimbali hapa jijini, Dar es Salaam zinashiriki katika shindano hilo.

Kikuli alisema shindano hilo limelenga kuwajengea uwezo wachoma nyama nchini kuandaa nyama katika hali ya ubora na usafi, huku akisisitiza bia hiyo imekuwa ikiandaa shindano hilo mara kwa mara.

Alisema kwa mwaka huu shindano hilo limeandaliwa kwa kuzingatia haki na kila baa ambayo majaji walikwenda walikuwa wakipata wasaha wa kuzungumza na wachoma nyama wa baa husika.

Aliongeza mshindi wa shindano hilo atapata zawadi ya Sh. milioni mbili pamoja na kupatiwa wasaha wa kushiriki katika shindano lingine la nyama choma litakalofanyika Desemba 4 hadi 5, mwaka huu, huku washiriki wengine watapatiwa vyeti vya ushiriki.

Majaji wa shindano hilo ni Fred Uisso, ambaye aliwahi kuiwakilisha nchi katika mashindano ya kimataifa ya mapishi, Mwaka 2016 alishinda shindano la dunia ya uchomaji nyama nchini Marekani na Hassanal Msiha ambaye ni Mkufunzi wa Chuo cha Zanzibar Transworld Academy, akijihusisha na masuala ya mapishi.

Michezo

Ijumaa Novemba 27, 2020

Nipashe




## KLOOP ALIA NA RATIBA YA EPL

HABARI UK 22



Pele



Maradona

# PELE: MARADONA

## ●●●Ipo siku tutacheza wote soka mbinguni...

**SAO PAULO, Brazil**

GWIJI wa soka la Brazil, Pele ametuma salamu za rambirambi kwa msiba wa nyota wa zamani wa Argentina, Diego Maradona, akitoa taarifa fupi akisema, "siku moja tutacheza pamoja mpira juu mawinguni."

Pele alitoa salamu hizo baada ya kifo hicho cha Maradona kilichotokea Jumatano na kusema anasikitika 'kumpoteza rafiki yake wa karibu'.

Maradona alifariki kwa mshtuko wa moyo akiwa na umri wa miaka 60.

Mwanasheria wa Maradona, alithibitisha gwiji huyo alifariki kutokana na matatizo hayo ya moyo.

"Pengine siku moja tutacheza pamoja mpira juu mawinguni," alisema Pele katika taarifa yake fupi iliyotolewa na wawakilishi wake na ikinukuliwa na Shirika la Habari la Reuters.

Maradona hivi karibuni alikuwa akikabiliwa na matatizo mengi ya kiafya huku akilazwa mara kadhaa.

Na Jumatano akiwa nyumbani kwake jijini Buenos Aires, mshindi huyo wa Kombe la Dunia mwaka 1986 akiwa na Argentina alifariki dunia kwa mshtuko wa moyo.

Raia wa Argentina, Alberto Fernandez ametangaza siku tatu za maombelezo ya kitaifa kutokana na kifo hicho cha Maradona.

Mapema mwezi huu, nyota huyo alifanyiwa upasuaji wa ubongo kwa ajili ya kutoa damu iliyoganda na baadaye akaruhusiwa kutoka hospitali wiki iliyopita.

Baada ya upasuaji huo, ilitangazwa kuwa Maradona angeanza matibabu ya uraibu wa pombe.

Maradona ni moja ya wachezaji bora zaidi wa kandanda kuwahi kutokea.

Mwaka 1986 akiwa nahodha wa Argentina, aliliongoza taifa lake kushinda Kombe la Dunia nchini Mexico huku akionyesha uwezo binafsi katika ushindi huo.

Alizichezea klabu za Barcelona ya Hispania na Napoli ya Italia.

Akiwa na Napoli alinyakua ubingwa wa Ligi Kuu Italia, Serie A, kwa misimu miwili.

Maradona aliifungia Argentina magoli 34 katika michezo 91, akishiriki michuano minne ya Kombe la Dunia.

Aliliongoza taifa lake katika fainali ya Kombe la Dunia la mwaka 1990 nchini Italia, ambapo walifungwa na iliyokuwa Ujerumani Magharibi.

Alikuwa tena nahodha wa taifa lake katika mashindano ya Kombe la Dunia mwaka 1994 nchini Marekani, lakini alirudishwa nyumbani baada ya kubainika alitumia dawa za kuongeza nguvu.

Katika miaka yake ya mwisho ya uchezaji aligubikwa na utumiaji wa dawa za kusisimua misuli pamoja na dawa za kulevya.

Maradona alitaabika na matumizi na uraibu wa dawa za kulevya aina ya cocaine na alifungiwa kucheza mpira kwa miezi 15 baada ya kubainika kuwa alikuwa akitumia dawa hizo mwaka 1991.

Alistaafu soka la kulipwa mwaka 1997 katika siku ya kuadhimisha miaka 37 ya kuzaliwa kwake, akiwa na klabu maarufu nchini Argentina ya Boca Juniors.

Maradona alichaguliwa kuwa Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Argentina mwaka 2008 na akaachana na kibarua hicho baada ya Kombe la Dunia mwaka 2010, ambapo Argentina ilitolewa na Ujerumani katika hatua ya robo fainali.

Baada ya hapo akaenda kuzinoa klabu kadhaa katika nchi ya Umoja wa Falme za Kiarabu na baadaye Mexico.

Mpaka umauti unamfika alikuwa na timu ya Gimnasia y Esgrima inayoshiriki Ligi Kuu nchini Argentina.

## `YANGA YATIMUA KOCHA AZAM FC

**Na Saada Akida**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, akisema uzito wa mabeki wa kati wa Azam FC ndio siri sababu kubwa ya kikosi chake kuibuka na ushindi, uongozi wa matajiri hao wa Chamazi umeachana na Kocha wao Mkuu, Aristica Cioaba.

Azam FC inatajwa kuachana na Cioaba ikiwa ni baada ya timu yake kupoteza mechi mbili mfululizo, ikianza na KMC na juzi ilipokea kichapo kingine kinachofanana cha bao 1-0 kutoka kwa Yanga.

Hata hivyo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam, Abdulkarim Amin 'Popat', hakupatikana jana kuelezea tetesi za kuvunja mkataba wa kocha huyo aliyekuwa anaiongoza timu hiyo akishirikiana na Mrundi Vivier Bahati.

Kaze alisema mchezo huo ulikuwa mzuri na ushindani mkubwa, hivyo alibadilisha mbinu kwa kuwapanga zaidi watu wenye kasi kutokana na alivyobaini tatizo la mabeki wa Azam kabla ya mechi hiyo.

"Yacouba (Sogne) na Kaseke (Deus), niliwapa jukumu sababu wao ni wepesi, Ditram Nchimbi alikuwa chaguo sahihi kwa sababu kabla ya uzito wa mabeki wa kati wa Azam," alisema Kaze.

Naye Vivier alisema mabeki wao hawakucheza vizuri katika kukaba huku Yanga ikiwazidi katika nafasi nyingi na kufanikiwa kuondoka na pointi tatu muhimu.

Alisema baada ya kutoka kwa mshambuliaji wao Prince Dube, aliyeumia, hali hiyo iliwavuruga huku Richard Djod kushindwa kufanya majukumu yake na kushindwa kutengeneza nafasi za mabao kama ilivyotarajiwa.

Kwa ushindi huo wa bao 1-0 kwa Yanga imefikisha pointi 28 na kukaa kileleni, huku Azam ikishuka hadi nafasi ya pili wakiwa na alama 25, timu hizo zikiwa zimecheza michezo 12 na mabingwa watetezi Simba wenye pointi 23 wakifuatia lakini wana mchezo mmoja mkononi.

Yanga itashuka tena dimbani kesho kuwakaribisha JKT Tanzania kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam wakati Azam FC watawafuata Biashara United katika mchezo utakaofanyika Jumatatu Novemba 30, mwaka huu Uwanja wa Karume mjini Musoma, Mara.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002